# Hotuba ya Lahore

*(Islam na dini nyingine za nchi hii)*

**Mwandishi**

**Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as]**

**wa Qadian**

**Mfasiri**

**Sheikh Yusufu Athumani Kambaulaya**

**AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT**
**TANZANIA**

**HOTUBA YA LAHORE**
Tafsiri ya Kiswahili

© Islam International Publications Ltd.

Chapa ya Kwanza ya Kiurdu: Qadian 1904
Chapa ya Kwanza ya Kiswahili: 2016
Nakala: 2000

Kimeenezwa na:
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mnazi mmoja, Dar es Salam.
Simu: +255222110473
Fax: +255222121744

Kimechapwa na:
Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salam, Tanzania
Simu: +255222111031

ISBN: 185372983-3

بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ

# MAELEZO YA MWENEZI

*"Islam na dini nyingine za nchi hii"* ni hotuba ya Seyyidna Ahmad[as], mwanzilishi mtukufu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadyya, iliyosomwa tarehe 3, Septemba 1904, mjini Lahore, katika mkutano mkubwa. Hotuba hii ilichapishwa kwa sura ya kitabu, na kwa mnasaba huo kimepewa jina *"Hotuba ya Lahore"* pia.

Seyyidna Ahmad[as] amethibitisha katika kitabu hiki ubora wa mafundisho ya dini ya Kiislam, akilinganisha na mafundisho ya Kibanyani na Kikristo. Akaandika kwamba sababu ya kuwa uwingi wa dhambi siku hizi ni upungufu wa utambuzi wa Mwenyezi Mungu. Na utambuzi huo hupatikana kwa kupata kuongea na Mwenyezi Mungu na dini zote zimefunga mlango wa maongezi na Mungu isipokuwa dini ya Kiislam. Mwishowe ameandika hoja za ukweli wa madai yake na matabiri yake yaliyotimia.

Sheikh Yusufu Athumani Kambaulaya wa Tanzania alifasiri kitabu hiki katika lugha ya Kiswahili. Kisha hapa Makao makuu katika *"Deski ya Kiswahili"* Sheikh Muzaffar Ahamd Durrani na Sheikh Mubarak Mahmud walirudia tafsiri hii sawa na matini ya Kiurdu ya kitabu hiki kwa uangalifu sana. Mwishoni Maulana Sheikh Jamil R. Rafiq aliboresha tafsiri hii kwa ustadi mkubwa. Aidha ndugu kadha wengine nao wakasaidia katika kukamilisha kazi hii, kama vile

Dkt. Muhammad Shafiq Sehgal, Sheikh Ansar Husain na Sharifu Tanwir Mujtaba.

Hao wote walioshughulikia kazi hii wanastahili kushukuriwa na kuombewa. Mwenyezi Mungu Awajaalie malipo bora na Akubali huduma yao. Amin.

**Chaudhry Muhammad Ali M.A.**
**Wakilut Tasnif, Tahrike Jadid.**
**Rabwah, Pakistan.**
**29 April 2009.**

**Leo kwa kusoma gazeti la ''*Pesa Akhbar*'',** toleo la 27 Agosti 1904, nimejua kuwa Mwirani mmoja aitwaye Hakim Mirza Mahmud anaishi mjini Lahore, na anamwunga mkono mdai mmoja wa umasihi, naye anataka ashindane nami. Mimi nasikitika kwamba sina nafasi kabisa, kwa hiyo siwezi kukubali ombi lake; kwani kesho, siku ya Jumamosi, ni siku ya mkutano ambamo nitakuwa na shughuli, na Jumapili asubuhi mapema nalazimika kwenda Gurdaspur kwa ajili ya kesi moja iliyofunguliwa mahakamani. Mimi nimekaa Lahore tangu siku kumi na mbili, katika kipindi hiki hakuna yeyote aliyeniletea ombi kama hili; sasa ninapojiandaa kuondoka na sina fursa ya hata dakika moja kwa shughuli nyingine, sielewi ombi hili katika wakati usiofaa lina maana gani na shabaha ipi. Lakini hata hivyo, namwarifu Bwana Hakim Mirza Mahmud kuwa ipo njia nyingine safi ya kukata shauri, nayo ni hii kuwa kesho tarehe 3 Septemba, makala yangu yatakayosomwa katika mkutano, makala hayo mhariri wa *Pesa Akhbar* ayachapishe katika gazeti lake kitimilifu. Namwomba Bwana Hakim aliyetajwa juu kwamba ayachapishe makala yake ya kupinga makala yangu katika gazeti hilo, kisha umma wenyewe utaamua baada ya kusoma makala haya mawili kuwa makala ya nani ni yenye msingi wa unyofu, kweli na dalili madhubuti, na makala ya nani hayakufikia daraja hilo. Nionavyo mimi, njia hii ya kuamua itakuwa salama sana isiyo na mabaya yanayotazamiwa katika mijadala mingi ya siku hizi. Bali kwa njia hii mazungumzo hayamwelekei Bwana Hakim wala yeye hajatajwa, hivyo makala ya aina hii

yatakuwa mbali na kusononesha ambako wakati mwingine hutokea katika majadiliano ya pamoja.

Wassalam,

Mwandishi,

**Mirza Ghulam Ahmad**

**wa Qadian.**

بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ

نَحۡمَدُہٗ وَ نُصَلِّیۡ عَلٰی رَسُوۡلِہِ الۡکَرِیۡمِ [1]

Kwanza namshukuru Yule Mungu Aliyetujaalia kuwa chini ya kivuli cha serikali yenye amani ambayo haituzuii kueneza dini yetu, na kwa uadilifu inaondoa kila mwiba kutoka katika njia yetu. Kwa hiyo, pamoja na kumshukuru Mungu tunaishukuru pia serikali hii.

Baada ya haya, enyi wasikilizaji waheshimiwa, wakati huu napenda kuongelea kidogo juu ya dini zilizomo katika nchi hii, na kadri niwezavyo nitazungumza kwa ustaarabu. Hata hivyo, naelewa kuwa kitabia baadhi ya watu wanachukizwa kusikiliza kweli ambazo ni kinyume cha itikadi na dini zao. Basi, jambo hili ni nje ya uwezo wangu kwamba niweze kuondoa chuki hiyo ya asili. Kwa vyovyote namwomba radhi kila mmoja kwa kueleza ukweli.

Enyi mabwana waheshimiwa! mimi baada ya kutafakari sana na baada ya kufunuliwa mfululizo wahyi wa Mungu nimejua kwamba ingawa katika nchi hii kuna madhehebu mengi mbalimbali na hitilafu za kidini zinaendelea kama mafuriko, hata hivyo jambo lisababishalo wingi wa hitilifu hiyo kwa kweli ni moja tu, nalo ni hili kuwa ndani ya watu wengi nguvu ya kiroho na kumwogopa Mungu imepungua, na nuru ya kimbinguni ambayo kwayo mtu anaweza kutofautisha haki na batili imetoweka kutoka katika mioyo mingi, na dunia inaendelea kuingiwa na fikira ya udaharia; yaani kwa vinywa

[1] Tunamhimidia Yeye na tunamsalia Mtume Wake Mtukufu[as]

vyao wanamtaja Mungu na Parmeshar[2] na mioyoni mwao fikira za kutomwamini Mungu zinaendelea kuzidi. Juu ya jambo hili upo ushahidi huu kwamba hali za kiamali si sawa kama ipasavyo. Yote yasemwa kwa ulimi, lakini hayatekelezwi kwa vitendo. Kama yuko mkweli fulani aliyefichikana, simshambulii katu, lakini hali zithibitikavyo kwa jumla ni kwamba shabaha ambayo kwayo mwanadamu amefungamanishwa na dini, shabaha hiyo imetoweka. Utakaso wa kweli wa moyo, mapenzi ya kweli kwa Mwenyezi Mungu, huruma ya kweli kwa ajili ya viumbe vyake, uvumilivu, huruma, uadilifu, unyenyekevu na khulka nyingine zote njema, ucha Mungu, utakaso na ukweli ulio kiini cha dini, watu wengi hawaelekei kwa huo. Ni masikitiko kuwa vita vya kidini vinaendelea kuzidi duniani siku hadi siku, lakini kiroho hali inaendelea kurudi nyuma. Shabaha hasa ya dini ni kumtambua Yule Mungu wa kweli Aliyeumba ulimwengu huu wote, na kufikia katika mapenzi yake daraja ambalo lateketeza mapenzi ya mwingine na kuhurumia viumbe vyake na kujipatia utakaso wa kweli. Lakini mimi naona kuwa shabaha hii katika zama hizi imesahaulika, na watu wengi wameshikamana na tawi mojawapo la dini ya Udaharia, na kumtambua Mwenyezi Mungu kumekuwa kidogo sana. Ndiyo maana siku hadi siku ujasiri wa kutenda maovu unaendelea kuongezeka, kwani ni jambo lisilokanika kuwa kitu kisichotambulikana, hakithaminiwi moyoni, wala hakipendwi wala hakihofiwi, maana hofu, upendo na thamini ya kitu, hayo yote hupatikana baada ya kukitambua. Basi, ni dhahiri kuwa siku hizi wingi wa

[2] Parmeshar ndiye Mungu kwa lugha ya Kihindi. (mfasiri)

dhambi duniani ni kwa sababu ya upungufu wa utambuzi. Na miongoni mwa alama za dini ya kweli, alama moja kubwa tukufu ni kwamba njia nyingi za kumtambua Mwenyezi Mungu na za kumjua ziwepo ndani yake ili mtu aweze kujizuia kufanya dhambi na ili kwa kutambua uzuri na jamali ya Mwenyezi Mungu apate sehemu ya mapenzi kamili na mahaba na ili aione hali ya kutengana na Mungu kuwa vibaya zaidi kuliko jahanamu. Ni jambo la kweli kuwa kuepukana na dhambi na kuzama katika mapenzi ya Mwenyezi Mungu ndiyo shabaha kubwa ya mwanadamu, na hiyo ndiyo raha ya kweli tunayoweza kuitafsiri kuwa ndiyo maisha ya peponi. Matamanio yote yaliyo kinyume cha radhi ya Mungu ni moto wa jahanamu, na kuishi katika kufuata matamanio hayo ni maisha ya kijahanamu. Lakini, lipo swali hapa kwamba kuna njia gani ya kujiokoa katika maisha haya ya kijahanamu? Kwa kulijibu hilo, elimu Aliyonijaalia Mungu ndiyo hii kuwa wokovu katika jahanamu hii unautegemea utambuzi wa Mungu ulio wa kweli na mkamilifu kwani jazba za kibinadamu zinazovuta upande wake ni mafuriko ya daraja kamili yanayopita kwa nguvu kuangamiza imani; na kukiondoa kitu kilichokamilika bila kilichokamilika ni muhali. Kwa sababu hii, kwa kupata wokovu, utambuzi kamili unahitajika; maana, hata kuna methali mashuhuri kuwa dawa ya moto ni moto. Jambo hili halihitaji hoja nyingi kuwa kuthamini kitu, kukipenda na kukihofu, mambo hayo yote yanazalika kwa kupata maarifa yaani utambuzi wa kitu hicho. Kama mtoto akipewa mkononi, mathalan, kipande cha almasi kinachoweza kuwa na thamani ya mamilioni ya rupia, lakini yeye ataithamini kiasi cha kukithamini kitu cha kuchezea

tu. Na mtu pasipo kujua akichanganyiwa sumu ndani ya asali, ataila asali hiyo kwa shauku kubwa na hataelewa kuwa ndani yake mna kifo chake. Maana, hana utambuzi wa sumu hiyo. Lakini nyinyi hamwezi kuingiza mkono kwa kusudi katika shimo la nyoka, kwani mnajua kuwa kufanya hivyo ni kuhatarisha maisha yenu. Vivyo hivyo, hamwezi kula sumu ya kuua kwa kusudi, kwani mnatambua kwamba mkiila sumu hiyo mtakufa. Basi kuna sababu gani hamkijali kifo kitakachowasibuni kwa kuvunja maagizo ya Mungu? Ni dhahiri kuwa sababu yake ndiyo tu kwamba nyinyi hamna utambuzi kama ule utambuzi mlio nao juu ya nyoka na sumu, yaani mnavitambua vitu hivyo. Ni hakika kabisa, na hakuna mantiki yoyote iwezayo kukataa ya kwamba utambuzi kamili unamzuia mwanadamu asitende matendo yamleteayo hasara ya maisha na mali. Na katika kujizuia huko mtu hahitaji kafara yoyote. Je, si kweli kuwa watu waovu pia waliozoea kufanya makosa hujizuia kutimiza maelfu ya tamaa zao za nafsi kwani kwa yakini wanajua kuwa watakamatwa papo hapo na kuadhibiwa vikali sana. Nanyi mnaona kwamba watu hao katika mchana hawawezi kuvamia, kwa kunyang'anya, maduka yaliyojaa maelfu ya rupia zilizoko wazi ambapo njiani kuna maishirini ya askari polisi wanaozunguka na silaha. Basi, je, watu hao wanajizuia kuiba au kunyang'anya kwa sababu wana imani imara juu ya kafara fulani au wanayo heba nyoyoni mwao ya itikadi ya msalaba? Hapana, bali kwa sababu tu kwamba wanatambua sare za rangi nyeusi za polisi, na mioyo yao inatetemeka kwa mng'aro wa panga zao; wanao utambuzi kamili kuwa wakibambwa kwa sababu ya kutumia nguvu, papo hapo watapelekwa jela. Kanuni hii, sio watu tu bali

hata wanyama pia wanaifuata. Simba yeyote anayeshambulia hawezi kuingia katika moto uwakao hata kama upande wa pili kuna windo. Hata mbwa mwitu hawezi kumshambulia mbuzi anayechungwa na mwenyewe aliye na bunduki iliyojaa risasi na upanga uliochomolewa. Basi, enyi wapendwa, hii ni falsafa ya kweli na iliyokwisha jaribiwa kwamba ili kujiepusha na dhambi mwanadamu anahitaji utambuzi kamili na siyo kafara yoyote. Nasema kweli kabisa kwamba kama kaumu ya Nuhu wangelikuwa na utambuzi mkamilifu unaozalisha hofu kamili, kamwe wasingeligharikі. Na kama kaumu ya Luti wangelijaaliwa utambuzi huo wasingelinyeshewa mawe. Na kama watu wa nchi hii wangejaaliwa utambuzi wa Mungu unaotetemesha mwili kwa hofu, maangamio ya tauni yaliyoifikia nchi hii yasingeifikia. Lakini utambuzi nakisi hauwezi kufaa hata kidogo, wala matokeo yake yaliyo hofu na upendo hayawezi kukamilika. Imani isiyo kamili haifai, na upendo usio kamili haufai, na hofu isiyo kamili haifai na utambuzi usio kamili nao haufai. Na kila mlo na mnywo usio kamili haufai. Je, katika hali ya njaa mnaweza kushiba kwa punje moja? Au mkiwa na kiu, je, mnaweza kutosheka na tone moja? Basi, enye wazembe katika kutia bidii, na wavivu katika kutafuta haki! nyinyi kwa utambuzi kidogo na kwa mapenzi kidogo na kwa hofu kidogo mwawezaje kutumaini kupata fadhili kubwa ya Mungu? Kutakasa katika dhambi ni kazi ya Mungu na kujaza mapenzi yake moyoni ni kazi ya huyo huyo Mwenye kudra na nguvu. Na kutia hofu ya adhama yake katika moyo hutokana na utashi wa Huyo Huyo. Na kanuni ya asili tangu kale imekuwa hivi kwamba hayo yote hupatikana baada ya utambuzi kamili. Na mzizi wa

hofu, upendo na kuthamini ni utambuzi uliokamilika. Basi yule aliyejaaliwa utambuzi mkamilifu amejaaliwa pia hofu na upendo kamili. Na yule aliyejaaliwa hofu na upendo kamili, huyu amejaaliwa wokovu katika kila aina ya dhambi inayozalika kwa sababau ya kujasiri. Basi, kwa wokovu huu hatuhitaji damu yoyote wala msalaba wowote wala hatuna haja ya kafara yoyote, bali tunahitaji kutoa dhabihu moja tu iliyo dhabihu ya nafsi yetu ambayo tabia yetu ya asili inahisi haja yake. Dhabihu hii kwa maneno mengine inaitwa Islam. Maana ya Islam ni kuweka shingo kwa ajili ya kuchinjwa, yaani kuweka, kwa ridhaa kamili, roho yako kwenye kizingiti cha Mungu. Jina hili zuri ni roho ya sheria yote na kiini cha maagizo yote. Kwa kuchinjwa, kuweka shingo mbele kwa furaha ya moyo na ridhaa, kunahitaji upendo mkamilifu na mahaba kamili. Na upendo kamili unataka utambuzi kamili. Hivyo, basi, neno Islam linaashiria kwenye jambo hili kwamba kwa dhabihu ya kweli kuna haja ya utambuzi kamili na upendo kamili, hamna haja ya kitu kingine. Kwenye habari hiyo Mwenyezi Mungu ndani ya Kurani Tukufu Anaashiria:

لَنْ يَّنَالَ اللّٰهَ لُحُوْمُهَا وَلَا دِمَآؤُهَا
وَلٰكِنْ يَّنَالُهُ التَّقْوٰى مِنْكُمْ [3]

Yaani, nyama (za dhabihu zenu) ha*zi*wezi kunifikia wala damu, bali dhabihu hii tu inanifikia kwamba mniogope Mimi na mshike utawa kwa ajili yangu.

Sasa yapasa kuelewa kuwa shabaha hasa ya maagizo ya dini ya Kiislamu ndiyo kwamba ule uhakika

[3] Al-Hajj: 38

uliofichika katika neno Islam ufikiwe. Kwa shabaha hiyo yamo mafundisho ndani ya Kurani Tukufu yanayojaribu kumfanya Mungu kuwa mpendwa, pengine huonyesha uzuri na jamali yake, na pengine hukumbusha hisani zake, kwani upendo wa mtu huingia moyoni ama kwa sababu ya uzuri, au kwa sababu ya hisani. Imeandikwa kuwa Mungu katika sifa zake zote njema Yu wa pekee, Hana mshirika, ndani yake hamna kasoro yoyote, Yu Mkusanyiko wa sifa zote njema zilizo kamili, Onyesho la nguvu zote tukufu, Chanzo cha viumbe vyote, na Chimbuko la upaji wote, Mmiliki wa malipo mema na adhabu, na mambo yote hurejea kwake. Yu karibu ijapokuwa Yuko mbali, na Yuko mbali ingawa Yu karibu, Yu juu ya vyote lakini haiwezi kusemwa kuna chochote chini yake. Amefichikana kuliko vitu vyote, lakini haiwezi kusemwa kuna kilicho dhahiri kuliko Yeye. Yu Hai Mwenyewe, na kila kitu kipo hai pamoja naye. Anajitegemea Mwenyewe na kila kitu chamtegemea Yeye. Amekibeba kila kitu, lakini hakuna kitu kilichombeba Yeye. Hakuna kitu kilichozalika chenyewe au kinachoweza kuishi chenyewe bila Yeye. Yeye Amekizunguka kila kitu, lakini haiwezi kusemwa ni mzunguko wa aina gani. Yu nuru ya kila kitu cha mbingu na ardhi, na kila nuru imeng'ara kwa Mkono Wake na ni kivuli cha Dhati Yake. Yeye ni Mola wa walimwengu, hakuna roho isiyolelewa naye na iliyojitegemea yenyewe. Hakuna nguvu yoyote ya roho yoyote isiyopatikana kutoka Kwake na kujiendesha yenyewe. Rehema zake ni za aina mbili. (1) Aina moja ndiyo rehema zinazoonekana tangu kale, bila mtendaji yeyote kutangulia kutenda amali yoyote, kama vile ardhi, mbingu, jua, mwezi, nyota, maji, moto, hewa na

chembechembe zote za ulimwengu huu zilizoandaliwa kwa ajili ya raha yetu; vivi hivi vitu vyote tulivyohitaji vimeandaliwa kwa ajili yetu kabla ya kuzaliwa kwetu; na hivi vyote viliandaliwa wakati ambapo sisi wenyewe hatukuwepo, wala kulikuwa hakuna amali yetu yoyote. Nani anaweza kusema kuwa jua limeumbwa kwa sababu ya kitendo changu? Au ardhi imeumbwa kwa sababu ya amali yangu fulani njema? Ilmuradi, hii ndiyo rehema iliyokwisha dhihiri kabla ya mtu na matendo yake ambayo si matokeo ya amali yoyote. (2) Rehema ya pili ni ile inayotokana na matendo na hakuna haja ya kuieleza. Kadhalika imo katika Kurani Tukufu kuwa Mungu Ameepukana na kila aibu na Yu mbali na kila upungufu, naye Anataka kwamba mwanadamu pia, kwa kufuata mafundisho Yake, aepukane na aibu. Na Anasema:

مَنْ كَانَ فِيْ هٰذِهٖٓ اَعْمٰى فَهُوَ فِي الْاٰخِرَةِ اَعْمٰى [4]

Yaani, mtu atakayekuwa kipofu katika dunia hii ambaye hatapata kumwona Yule Asiye na mfano, huyo baada ya kufa pia atakuwa kipofu na giza halitatengana naye, kwani katika dunia hii hii mtu hupewa hisia za kumwona Mungu, na yule mtu ambaye hataenda na hisia hizo kutoka duniani, huko akhera pia hataweza kumwona Mungu. Katika aya hii Mwenyezi Mungu Amefahamisha kwa uwazi kabisa kuwa Yeye Anataka maendeleo gani kutoka kwa mwanadamu, na kwamba kwa kufuata mafundisho yake mtu anaweza kufika mpaka wapi. Kisha baada yake Anaeleza katika Kurani Tukufu mafundisho ambayo kwa kuyafuata na kuyatekeleza

---

[4] Bani Israil: 73

mtu anaweza kumshuhudia Mungu, kama Anavyosema:

مَنْ كَانَ يَرْجُوْا لِقَآءَ رَبِّهٖ فَلْيَعْمَلْ عَمَلًا
صَالِحًا وَّلَا يُشْرِكْ بِعِبَادَةِ رَبِّهٖٓ اَحَدًا ۝ [5]

Yaani, mtu anayependa apate bahati ya kumwona Mungu katika dunia hii hii Ambaye ni Mungu wa kweli na Mwumbaji, basi yampasa atende matendo mema yasiyo na ufisadi wowote ndani yake, yaani matendo yake yasiwe kwa kuwaonyesha watu, wala yasisababishe kiburi kuzalika moyoni kuwa mimi niko hivi na hivi, wala matendo hayo yasiwe na nakisi na kasoro wala yasiwe na harufu mbaya ndani yake iliyo dhidi ya upendo hasa; bali yapasa yawe yamejaa ukweli na unyofu. Pamoja na hayo yapasa kujiepusha na kila aina ya ushirikina. Lisichukuliwe jua wala mwezi wala nyota za mbinguni wala hewa wala moto wala maji wala kitu kingine chochote cha ardhini kuwa kitu cha kuabudiwa; wala njia za kidunia zisipewe heshima, wala zisitegemewe kiasi hiki kana kwamba hizo ni washiriki wa Mungu, wala nguvu na juhudi yetu isihesabiwe kuwa chochote, maana hii pia ni aina mojawapo ya ushirkina, bali baada ya kutia juhudi yote ifahamike kwamba hatujafanya kitu, wala tusijivunie elimu yetu wala tusione fahari kwa matendo yetu. Bali tujihesabu kwa kweli majahili na tujione tu wavivu, na wakati wote roho iwe inaanguka juu ya kizingiti cha Mwenyezi Mungu, na tuvutie baraka za Allah kwa maombi. Na tuwe kama mtu ambaye ni mwenye kiu tena hana mikono wala miguu, na mbele yake chemchem moja imedhihirika

[5] Al-Kahf :111

ya maji safi sana na matamu, naye baada ya kujikokota kwa vyovyote akajifikisha kwenye chemchem hiyo, akaweka midomo yake kwenye chemchem hiyo, na hakujiondoa hadi akatosheka. Na kisha Mungu wetu ndani ya Kurani Tukufu Anasema kuhusu sifa zake:

قُلْ هُوَ اللّٰهُ اَحَدٌ ۚ اَللّٰهُ الصَّمَدُ ۚ
لَمْ يَلِدْ ۙ وَلَمْ يُوْلَدْ ۙ وَلَمْ يَكُنْ لَّهٗ كُفُوًا اَحَدٌ [6]

Yaani, Mungu wenu ni yule Mungu Ambaye Yu Mmoja katika dhati yake na sifa zake. Hakuna dhati yoyote ya azali wala ya abadi — yaani isiyo na mwanzo wala mwisho — kama Yeye wala sifa za kitu chochote hazifanani na sifa Zake.

Elimu ya mwanadamu inamhitaji mwalimu, tena ina kikomo; lakini elimu Yake haimhitaji yeyote, na juu ya hayo haina mipaka. Kusikia kwa mtu kunahitaji hewa na kuna mipaka, lakini kusikia kwa Mungu ni kwa nguvu yake binafsi na hakuna mipaka. Kuona kwa mwanadamu kunahitaji jua au mwanga mwingine wowote na kuna mipaka, lakini kuona kwa Mungu ni kwa mwanga Wake binafsi na haina mipaka. Vivyo hivyo nguvu ya mwanadamu kuzaa inahitaji maada fulani, na inahitaji muda, tena ina mpaka; lakini uwezo wa Mungu kuumba hauhitaji maada yoyote, wala hauhitaji muda wala hauna mipaka. Kwani sifa zake zote hazina mfano. Na jinsi ambavyo Hana mfano, kadhalika sifa zake nazo hazina mfano. Kama Yeye ana kasoro katika sifa moja, basi Yeye atakuwa na kasoro katika sifa zote. Kwa hiyo, Umoja Wake hauwezi kuwepo mpaka

[6] Ikhlas :2-5

Yeye sawa na dhati yake asiwe na mfano wala mithili yake katika sifa zake zote pia. Kisha tafsiri ya maneno ya baadaye ya aya iliyotajwa hapo juu ni hii kwamba Mungu si mwana wa yeyote wala hakuna yeyote aliye mwanaye. Kwani Yeye ni mkwasi katika dhati yake, Hana haja ya baba wala ya mwana. Huu ndio Umoja uliofundishwa na Kurani Tukufu ambao ndio msingi wa imani. Na kuhusiana na matendo, aya hii kamilifu imo katika Kurani Tukufu:

إِنَّ اللّٰهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالْإِحْسَانِ وَإِيْتَآئِ ذِي
الْقُرْبٰى وَيَنْهٰى عَنِ الْفَحْشَآءِ وَالْمُنْكَرِ وَالْبَغْيِ[7]

Yaani, Mungu Anawaamuruni kuwa fanyeni uadilifu na mwimarike juu ya adili. Na kama mkitaka kukamilika zaidi ya hayo, basi fanyeni hisani, yaani watendeeni vizuri na kuwafanyia wema watu ambao hawakuwafanyieni wema wowote. Na kama mkitaka kuwa wakamilifu zaidi, basi wafanyieni wema wanadamu kwa huruma yenu halisi na kwa jazba ya asili bila kudhamiria kushukuriwa au kuwafanya watambue kwamba wamefanyiwa hisani, kama vile mama anavyomfanyia wema mwanaye kwa sababu tu ya uharara wa asili. Asema: Mwenyezi Mungu Anawakatazeni kudhulumu au kusimbulia au kutomshukuru mwenye kuwafanyieni huruma ya kweli. Na Akifafanulia aya hii Anasema mahali pengine:

وَيُطْعِمُوْنَ الطَّعَامَ عَلٰى حُبِّهٖ مِسْكِيْنًا وَّيَتِيْمًا وَّ أَسِيْرًا ۝
إِنَّمَا نُطْعِمُكُمْ لِوَجْهِ اللّٰهِ لَا نُرِيْدُ مِنْكُمْ جَزَآءً وَّلَا شُكُوْرًا ۝ [8]

[7] Kwa hakika Mwenyezi Mungu Anaamuru uadilifu, na hisani, na kuwapa (watu kama uwapavyo) ndugu; na Anakataza upujufu, na uovu, na uasi. Al-Nahl : 91

Yaani, waaminifu wakamilifu wanapowalisha chakula wenye hali ndogo na mayatima na wafungwa, huwalisha kwa sababu ya mapenzi tu ya Mungu, si kwa shabaha nyingine yoyote ile, na wanawaambia kuwa huduma hii ndiyo kwa ajili ya Mungu tu, hatutaki malipo yake yoyote na wala hatutaki mtutolee shukurani. Kisha kuhusiana na adhabu na malipo Kasema:

جَزٰٓؤُا سَيِّئَةٍ سَيِّئَةٌ مِّثْلُهَا فَمَنْ عَفَا وَاَصْلَحَ فَاَجْرُهٗ عَلَى اللّٰهِ [9]

Yaani, malipo ya ubaya ni ubaya uliosawa nao. Jino kwa jino na jicho kwa jicho, tusi kwa tusi. Na yule mtu anayesamehe lakini msamaha ule ulete urekebisho sio uharibifu, yaani aliyesamehewa ajirekebishe na ajiepushe na uovu, hapo msamaha ukitolewa kwa sharti hilo utakuwa bora kuliko kulipiza kisasi, na mwenye kusamehe atapata malipo yake mema. Siyo kwamba baada ya kupigwa kofi shavu moja, ligeuzwe tu la pili pia mahali pafaapo au pasipofaa; hii ni kinyume cha hekima. Na baadhi ya wakati wabaya kuwafanyia wema hudhuru kana kwamba umewafanyia watu wema ubaya. Na Kasema tena:

اِدْفَعْ بِالَّتِیْ هِیَ اَحْسَنُ فَاِذَا الَّذِیْ بَیْنَكَ وَبَیْنَهٗ عَدَاوَةٌ كَاَنَّهٗ وَلِیٌّ حَمِیْمٌ ○ [10]

Yaani, kama mtu akikufanyia wema, wewe mfanyie wema zaidi kuliko yeye. Ikiwa utafanya hivyo, hata

---

[8] Ad-Dahr : 9-10

[9] Ash-Shura : 41

[10] Zuia ubaya kwa yaliyo mema zaidi, na mara yule ambaye baina yako na yeye pana uadui atakuwa kama ni rafiki sana. Haa Miim As-Sajdah : 35

kama kuna uadui baina yenu, huo utabadilika kuwa urafiki kana kwamba yeye mtu huyo ni rafiki pia na jamaa vile vile. Na Akasema:

وَلَا يَغْتَبْ بَّعْضُكُمْ بَعْضًا ؕ اَيُحِبُّ اَحَدُكُمْ اَنْ يَّاْكُلَ لَحْمَ اَخِيْهِ مَيْتًا [11]

لَا يَسْخَرْ قَوْمٌ مِّنْ قَوْمٍ عَسٰٓى اَنْ يَّكُوْنُوْا خَيْرًا مِّنْهُمْ [12]

اِنَّ اَكْرَمَكُمْ عِنْدَ اللّٰهِ اَتْقٰكُمْ ؕ [13]

وَلَا تَنَابَزُوْا بِالْاَلْقَابِ ؕ بِئْسَ الِاسْمُ الْفُسُوْقُ بَعْدَ الْاِيْمَانِ [14]

فَاجْتَنِبُوا الرِّجْسَ مِنَ الْاَوْثَانِ وَ اجْتَنِبُوْا قَوْلَ الزُّوْرِ ○ [15]

وَقُوْلُوْا قَوْلًا سَدِيْدًا ○ [16]

وَاعْتَصِمُوْا بِحَبْلِ اللّٰهِ جَمِيْعًا [17]

Yaani, yapasa mmoja wenu asimtete mwenzake. Je mmoja wenu anapenda kula nyama ya nduguye aliyekufa? Na inatakiwa taifa moja lisilicheke taifa jingine kuwa eti kabila letu ni aali kuliko lao; huenda wao wakawa bora kuliko nyinyi; na mbele ya Mungu aheshimiwaye sana ni yule aliye mwema na mtawa zaidi. Tofauti za mataifa si chochote wala lolote. Na msiwaite watu kwa majina yanayowachukiza au wanayoona yanawavunjia heshima; la sivyo, mbele ya Mungu jina lenu litakuwa fasiki. Jiepusheni na masanamu na uongo, maana hivi viwili ni vichafu. Mnapoongea, ongeeni kwa kutumia hekima na akili,

---

[11] Al Hujuraat : 13

[12] Al Hujuraat : 12

[13] Al Hujuraat :14

[14] Al Hujuraat : 12

[15] Al-Hajj : 31

[16] Al-Ahzab : 71

[17] Aali ‘Imrani : 104

na mjiepushe na upuuzi. Na yawapasa viungo vyenu vyote na nguvu zenu zote zimtii Mungu, nanyi nyote mkiwa pamoja Mtiini Yeye. Na kisha Akasema mahali pengine:

اَلْهٰكُمُ التَّكَاثُرُ ۙ○ حَتّٰى زُرْتُمُ الْمَقَابِرَ ○ۗ كَلَّا سَوْفَ تَعْلَمُوْنَ ۙ○
ثُمَّ كَلَّا سَوْفَ تَعْلَمُوْنَ ○ۗ كَلَّا لَوْ تَعْلَمُوْنَ عِلْمَ الْيَقِيْنِ ○ۗ لَتَرَوُنَّ
الْجَحِيْمَ ۙ○ ثُمَّ لَتَرَوُنَّهَا عَيْنَ الْيَقِيْنِ ۙ○ ثُمَّ لَتُسْـَٔلُنَّ يَوْمَئِذٍ عَنِ النَّعِيْمِ ○ [18]

Enyi watu mlioghafilika na Mungu, hamu ya dunia imewaghafilisheni mpaka mnaingia makaburini na hamwachi mghafala; hili ni kosa lenu, na karibuni mtajua, tena nasema karibuni mtajua. Mkipata elimu ya yakini, mtaona Jahanamu yenu kwa kutafakari kwa njia ya elimu, ndipo mtajua kwamba maisha yenu ni ya kijahanamu. Na kama mkipata utambuzi zaidi, mtaona kwa jicho la yakini kamili kwamba maisha yenu ni ya kijahanmu. Kisha wakati ule pia utawadia ambapo mtatupwa katika jahanamu na mtaulizwa juu ya kila anasa na kupita kiasi, yaani kwa kushikwa na adhabu mtaifikia haki ya yakini (yakini barabara). Ndani ya aya hizo jambo hili linaashiriwa kuwa yakini ziko za aina tatu. Ya kwanza inapatikana kwa elimu na kwa kukisia tu kama vile mtu aone moshi kutoka mbali, na kwa kukisia na kutumia akili atambue kwamba lazima kule kuna moto. Na aina ya pili ya yakini ni hii kwamba auone moto huo kwa macho yake. Na aina ya tatu ya yakini ni hii kwamba, kwa mfano, aweke mkono ndani ya moto huo akaonje ladha ya nguvu yake ya kuunguza. Basi hizi ndizi aina tatu: (1) Elimu ya yakini. (2) Jicho la yakini. (3) Ukweli wa yakini. Katika aya hii, Mwenyezi Mungu

[18] At-Takaathur : 2-9

Amefahamisha kuwa raha yote ya mtu imo katika ukaribu na upendo wa Mwenyezi Mungu; na pale mtu anapovunja uhusiano naye na kuinamia dunia, basi haya ni maisha ya kijahanamu. Na kila mtu hatimaye anagundua maisha ya kijahanamu, ingawa ayagundue wakati akaribiapo kufa akiachana mara moja na mali na vifaa na uhusiano wa dunia. Kisha mahali pengine katika Kurani Tukufu Mwenyezi Mungu Anasema:

وَلِمَنْ خَافَ مَقَامَ رَبِّهٖ جَنَّتٰنِ ○ [19]

Yaani, mtu akijali enzi na heshima ya Mwenyezi Mungu na akihofia kwamba siku moja ataulizwa mbele ya Mungu, anaiacha dhambi, atapatiwa pepo mbili. (1) Ya kwanza, atapatiwa katika dunia hii hii maisha ya peponi na yatatokea mabadiliko matakatifu ndani yake, na Mungu Atakuwa Msimamizi na Mkimu wake. (2) Ya pili, atapewa pepo ya milele baada ya kufa. Hiyo ni kwa sababu akamcha Mungu na akamtanguliza juu ya dunia na tamaa za nafsi. Kisha mahali pengine katika Kurani Tukufu Anasema:

اِنَّآ اَعْتَدْنَا لِلْكٰفِرِيْنَ سَلٰسِلَاۡ وَاَغْلٰلًا وَّسَعِيْرًا ○ اِنَّ الْاَبْرَارَ يَشْرَبُوْنَ مِنْ
كَاْسٍ كَانَ مِزَاجُهَا كَافُوْرًا ○ عَيْنًا يَّشْرَبُ بِهَا عِبَادُ اللّٰهِ يُفَجِّرُوْنَهَا تَفْجِيْرًا ○ [20]
وَيُسْقَوْنَ فِيْهَا كَاْسًا كَانَ مِزَاجُهَا زَنْجَبِيْلًا ○ عَيْنًا فِيْهَا تُسَمّٰى سَلْسَبِيْلًا ○ [21]

Yaani, kwa ajili ya makafiri wasio na upendo wetu moyoni na walioelekea dunia, Tumewaandalia minyororo na ukosi wa chuma wa shingoni na njia za kuchoma nyoyo. Na minyororo ya huba ya dunia imo miguuni mwao, na shingoni wanayo kola ya chuma

[19] Ar-Rahman : 47

[20] Al-Dahr : 5-7

21 Al-Dahr : 18-19

ya kuachana na Mungu ambayo kwayo hawawezi kutazama juu wakiinua kichwa, na wanaedelea kuangukia dunia. Na kila wakati wanayo dukuduku moyoni mwao kwa ajili ya matamanio ya dunia. Lakini wafanyao wema wanaendelea kunywa katika dunia hii hii sharubati ya kafuri iliyopoza mahaba ya dunia katika mioyo yao na imemaliza kiu ya kutafuta dunia. Ni chemchemi ya sharubati ya kafuri wanayopewa, nao wakiipasua pasua chemchemi hii wanaifanya kuwa mto ili wawashirikishe wenye kiu wa karibu na wa mbali. Na chemchemi hiyo inapokuwa katika sura ya mto, na nguvu ya imani inapozidi na mapenzi ya Mungu yanapoanza kukua, ndipo sharubati nyingine wananyweshwa inayoitwa sharubati ya tangawizi. Yaani kwanza wao hunywa sharubati ya kafuri ambayo kazi yake ni kupoza tu mapenzi ya kidunia ndani ya mioyo yao, lakini baada ya hapo wanahitaji sharubati ya moto ili joto la mapenzi ya Mungu lichemke ndani yao kwani kuacha tu uovu sio ukamilifu. Basi hiyo inaitwa sharubati ya tangawizi, na chemchemi hiyo yaitwa Salsabil, maana yake "Ulizia njia ya Mungu". Kisha mahali pengine Anasema:

قَدْ اَفْلَحَ مَنْ زَكّٰىهَا ۝ وَقَدْ خَابَ مَنْ دَسّٰىهَا ۝ [22]

Yaani, mtu yule amejiokoa katika tamaa za nafsi na amepata maisha ya peponi, aliyeitakasa nafsi yake; na ameshindwa kabisa yule mtu ambaye aliifukia nafsi yake na hakuelekea mbinguni. Na kwa kuwa madaraja hayo hayawezi kupatikana kwa juhudi peke yake ya mwanadamu, ndiyo maana katika sehemu

[22] Ash-Shams: 10-11

mbalimbali za Kurani Tukufu Ameshawishi kufanya maombi na juhudi kama Anavyosema:

اُدۡعُوۡنِیۡۤ اَسۡتَجِبۡ لَکُمۡ ؕ [23]

Yaani, ombeni, nami nitawapokeleeni maombi yenu. Na Anasema tena:

وَ اِذَا سَاَلَکَ عِبَادِیۡ عَنِّیۡ فَاِنِّیۡ قَرِیۡبٌ ؕ اُجِیۡبُ دَعۡوَۃَ الدَّاعِ
اِذَا دَعَانِ ۙ فَلۡیَسۡتَجِیۡبُوۡا لِیۡ وَ لۡیُؤۡمِنُوۡا بِیۡ لَعَلَّہُمۡ یَرۡشُدُوۡنَ ○ [24]

Yaani, kama watumishi wangu wakiuliza juu yangu kwamba kunathibitikaje kuwepo Kwake, na tufahamuje kwamba Mungu Yupo, basi jibu lake ni hili kuwa Mimi Nipo karibu sana. Mimi namjibu anayeniita, na anaponiita nasikia sauti yake na kuongea naye. Kwa hiyo, yawapasa wawe hivi kwamba Mimi Niweze kuongea nao, nao waniamini kikamilifu ili waipate njia yangu. Anasema tena:

وَ الَّذِیۡنَ جَاہَدُوۡا فِیۡنَا لَنَہۡدِیَنَّہُمۡ سُبُلَنَا ؕ [25]

Yaani, wale wanaojibidiisha na kujitahidi kwa namna mbalimbali katika njia yetu na kwa kututafuta Sisi huwaonyesha njia yetu.

Asema tena:

وَ کُوۡنُوۡا مَعَ الصّٰدِقِیۡنَ ○ [26]

Yaani, kama mnataka kukutana na Mungu, basi fanyeni maombi na jitahidini vile vile na suhubianeni pia na wakweli; maana katika njia hii suhuba pia ni

[23] Al-Mumin: 61

[24] Al-Baqara: 187

[25] Al-Ankabuut: 70

[26] At-Tauba: 119

sharti. Hukumu hizo zote ndizo zinazomfikisha mtu kwenye uhakika wa Islam. Kwani, kama nilivyokwisha eleza, uhakika wa Uislamu ni mtu kuweka shingo yake mbele ya Mwenyezi Mungu kama mbuzi wa dhabihu; na kuliliwala makusudio yake yote na kushughulikia katika utashi na ridhaa ya Mungu; na kwa kujipoteza ndani ya Mungu kukubali mauti; na kwa kujipatia mapenzi yake hasa makamilifu kumtii kwa jazba ya mapenzi tu wala si kwa sababu nyingine yoyote; na kupata macho yanayoona pamoja na Mungu tu, na kupata masikio yanayosikia pamoja naye; na kufanyiza moyo wenye kumwelekea Yeye moja kwa moja; na kupata ulimi unaotamka Atamkishapo Yeye. Hapo ndipo panapoishia juhudi zote na nguvu za kibinadamu zinamaliza kazi zote zilizokuwa juu yao, na tamaa za nafsi za mtu zinajifia kikamilifu, ndipo rehema ya Mwenyezi Mungu, kwa neno lake hai na nuru zake zinazong'aa inamhuisha mara nyingine, naye hujaaliwa neno tamu la Mungu, na nuru ile isiyoelezeka ambayo akili haiwezi kuitambua wala macho hayaufikii uhakika wake, hiyo yenyewe inamsogelea mtu moyo wake kama Asemavyo Mungu:

نَحۡنُ اَقۡرَبُ اِلَیۡہِ مِنۡ حَبۡلِ الۡوَرِیۡدِ ○ [27]

Yaani, Sisi Tuko karibu naye zaidi kuliko hulkumu yake. Basi yeye Anamjaalia mtu mwenye asili ya kufa heshima ya ukaribu wake. Ndipo ujapo wakati ambapo upofu unatoweka na macho yanapata mwanga na mwanadamu anamwona Mungu wake kwa macho yake haya mapya, na anasikia sauti yake, anajikuta amefunikwa ndani ya shuka la nuru Yake,

[27] Qaaf:17

ndipo shabaha ya dini inafikia kikomo, na mwanadamu kwa kumshuhudia Mungu wake anatupilia mbali joho chafu la maisha duni kutoka mwili wake na anajivalia mavazi ya nuru, na si kwa sababu tu ya ahadi wala si kwa kungojea akhera anaendelea kusubiri kumwona Mungu na pepo, bali hapa hapa na katika hii hii dunia anamwona Yeye na kuzungumza naye na kupata neema za peponi, kama vile Mwenyezi Mungu Anavyosema:

إِنَّ الَّذِينَ قَالُوا رَبُّنَا اللّٰهُ ثُمَّ اسْتَقَامُوا تَتَنَزَّلُ عَلَيْهِمُ الْمَلٰٓئِكَةُ
أَلَّا تَخَافُوا وَلَا تَحْزَنُوا وَأَبْشِرُوا بِالْجَنَّةِ الَّتِي كُنْتُمْ تُوعَدُونَ ○ [28]

Yaani, wale wanaosema kuwa Mungu wetu ni Mungu Mwenye sifa zote zilizo kamili, Asiye na mshirika yeyote katika dhati yake na sifa zake, na baada ya kutamka hivi wanadumisha hali hiyo. Na hata kama matetemeko mengi namna gani yatokee na mabalaa yashuke na mauti yawakabili, hakuna tofauti yoyote inayotokea ndani ya imani na ikhlasi yao. Malaika huwateremkia na Mungu Huongea nao na Huwaambia msiyaogope mabalaa wala msiwaogope maadui wakali wala msihuzunike juu ya misiba iliyopita. Mimi niko pamoja nanyi, nami ninawapeni pepo mliyokuwa mkiahidiwa katika dunia hii hii, basi ifurahieni. Sasa ibainike kuwa maneno hayo siyo pasipo ushahidi, na ahadi hizo siyo kwamba hazikutimia, bali maelfu ya wenye mioyo safi katika dini ya Kiislamu wameisha onja ladha ya pepo hiyo ya kiroho. Kwa kweli Islam ndiyo dini ambayo wafuasi wake wakweli Mwenyezi Mungu Amewafanya warithi wa wakweli wote wa zamani na

[28] Ha-Mim: 31

Ameupatia neema zao mbalimbali umati huu mrehemiwa na Amekubali dua hii Aliyofundisha Mwenyewe ndani ya Kurani Tukufu, nayo ndiyo hii:

اِهۡدِنَا الصِّرَاطَ الۡمُسۡتَقِيۡمَ○صِرَاطَ الَّذِيۡنَ
اَنۡعَمۡتَ عَلَيۡهِمۡ ۙ غَيۡرِ الۡمَغۡضُوۡبِ عَلَيۡهِمۡ وَلَا الضَّآلِّيۡنَ○ [29]

Utuongoze njia ambayo ndiyo njia ya wakweli Uliowapatia kila aina ya neema, yaani wale waliopata baraka za kila aina kutoka Kwako na wamepata heshima ya kuongea nawe, na wamekubaliwa maombi; na wakajaaliwa nusura na msaada na uongozi wako. Na tuepushe na njia za wale waliopata ghadhabu yako, na kwa kuacha njia yako wakafuata njia zingine. Hii ni dua inayoombwa mara tano katika sala. Na hii inaeleza kuwa katika hali ya upofu, maisha ya dunia pia ni jahanamu moja, tena kufa pia ni jahanamu moja, na kwa hakika mtii wa kweli wa Mungu na mwenye kupata wokovu kwa kweli anaweza kuwa yule tu anayemtambua Mungu na kumwamini kikamilifu, na ndiye anayeweza kuacha dhambi na kujisahau katika mapenzi ya Mungu. Kwa hiyo, moyo usio na hamu na utashi wa kupata kuongea na Mungu kwa yakini, moyo huo ni mfu. Na dini isiyo na uwezo wa kufikisha kwenye ukamilifu huo na kuwafanya wafuasi wake wakweli waongee na Mungu, dini hiyo haikutoka kwa Mungu wala haina roho ya kweli ndani yake. Vivyo hivyo nabii yeyote ambaye hakuwaelekeza watu kwenye njia hii kwamba wawe na utashi wa kuongea na Mungu, na wapende kupata utambuzi kamili, nabii huyo naye hakutoka kwa Mungu, bali anamtungia Mungu uongo. Kwani

[29] Al-Fatiha: 6-7

shabaha kubwa ya mwanadamu ambayo kwayo yeye anaweza kujiokoa katika dhambi ndiyo hii kuwa awe na yakini kamili ya kuwepo kwa Mungu na adhabu yake na malipo yake. Lakini itapatikanaje yakini juu ya kuwepo kwa Mungu Aliyefichikana kabisa pasipo kusikika sauti kutoka Kwake isemayo "Anal Maujuud" (Mimi Nipo)! Na bila mtu kuzishuhudia kutoka Kwake ishara wazi wazi kabisa, itapatikanaje yakini kamili juu yake!! Kugundua kuwepo kwa Mungu kwa hoja za akili ni mpaka kiwango hiki tu kwamba akili timamu, baada ya kuona ardhi na mbingu na taratibu yake nzuri kabisa na imara, inapendekeza kwamba vitu hivyo vyenye hekima vinatakiwa kuwa na mtengenezaji, lakini haiwezi kuonyesha kwamba mtengenezaji kwa kweli yupo. Na ni dhahiri kwamba "anatakiwa kuwepo" ni wazo tu na "yupo" ni jambo la hakika; na kuna tofauti dhahiri shahiri baina ya hayo mawili. Yaani, katika hali ya kwanza imeelezwa haja tu ya mtengenezaji, na katika hali ya pili inatolewa ushahidi wa kuwepo kwake kwa kitendo. Ilmuradi, katika zama hizi kuna mafuriko makali ya mashindano baina ya dini mbalimbali. Mtafutaji haki anapaswa asisahau shabaha hii ya msingi kuwa dini ya kweli ni ile inayoweza kuonyesha Mungu kwa yakini kamili na kuweza kufikisha kwenye daraja la kuongea na Mungu na kumwezesha mtu aongee na Mungu, na kwa njia hii inaweza kwa nguvu yake ya kiroho na sifa ya kulea roho, kuokoa mioyo katika giza la dhambi; na minghairi ya hiyo, nyinginezo zote ndizo zidanganyazo tu. Sasa twaziangalia dini chache za nchi hii kuwa je, hizi zinaweza kufikisha kwenye yakini kamili ya utambuzi wa Mwenyezi Mungu, na je, ndani ya vitabu vyao imo ahadi ya kuwa hizo

zinaweza kumwezesha mtu kufanya maongezi ya yakini na Mungu? Na kama imo, basi, je, ipo yoyote katika dini hizo iliyotimiza pia ahadi hiyo katika zama hizi au hapana? Basi, kwanza kabisa dini inayostahili kutajwa ni ile inayoitwa dini ya Kikristo. Ibainike kwamba hatuna haja ya kuandika sana kuhusu dini hii kwa vile Wakristo wenyewe wameisha afikiana juu ya jambo hili kuwa baada ya zama za Yesu ufunuo na wahyi umekoma, sasa neema hii haiendelei tena, bali imebakia nyuma, na sasa hakuna njia yoyote ya kuipata, na mpaka siku ya kiama hakuna matumaini, na mlango wa neema umefungwa; labda ndiyo sababu kwamba kwa kupata wokovu imebuniwa njia nyingine, na imeshauriwa tiba nyingine mpya ambayo ni ngeni kwa kanuni ya dunia nzima na ni kinyume cha akili, uadilifu na huruma, nayo ni hii kwamba inasemekana kuwa bwana Yesu akichukua madhambi yote ya dunia nzima akakubali kufa msalabani ili kwa sababu ya kifo chake hiki wengine wapate kuokoka. Mungu Akamwua mwanaye asiyekuwa na hatia ili kuwaokoa wenye dhambi. Lakini hatuelewi kabisa kwamba kwa kifo cha aina hii cha kudhulumiwa, mioyo ya wengine inawezekanaje kutakata na kutakasika na tabia chafu ya dhambi? Na inawezekanaje kwa mauaji ya mtu mmoja asiyekuwa na hatia watu wengine wapate hati ya kusamehewa madhambi yao yaliyopita, bali kwa njia hii uadilifu na huruma vyote viwili vinapotezwa kwa vile kumkamata asiye na dhambi badala ya mwenye dhambi ni kinyume cha uadilifu. Aidha kumwua mwana kwa njia hii bila haki na kwa ukatili ni kinyume cha huruma, tena kitendo hiki hakina faida yoyote. Sasa hivi tumeisha andika kuwa sababu yenyewe ya mafuriko ya dhambi ni

upungufu wa utambuzi. Hivyo, maadamu sababu ipo basi matokeo yake hayawezi kukatalika; daima sababu inahitaji matokeo yake. Sasa jambo la kushangaza ni kuwa falsafa hii ni ya aina gani kwamba sababu ya kutenda dhambi ─ iliyo upungufu wa utambuzi wa Mungu ─ ipo pale pale, lakini matokeo yake, ambayo ni hali ya kutenda dhambi, yametoweka. Uzoefu unatupa maelfu ya mashahidi kuwa bila utambuzi kamili, upendo wa kitu chochote hauwezi kupatikana wala hofu ya kitu chochote haipatikani na wala kitu chenyewe hakithaminiwi. Na hii ni wazi kuwa mtu hutenda kitendo au kuacha kutenda kitendo kwa hofu au kwa upendo; hofu na upendo vyote viwili vyapatikana kutokana na utambuzi. Basi kama hakuna utambuzi, hakuna hofu wala upendo.

Enyi ndugu wapenzi, hapa kuuhami ukweli kunatulazimisha kueleza kwamba Wakristo hawana mikononi mwao jambo lolote wazi kuhusu utambuzi wa Mwenyezi Mungu. Njia ya wahyi imefungwa tayari, na miujiza nayo imekoma baada ya Yesu na wanafunzi wake. Iliyobaki ni njia ya kutumia akili; basi njia hiyo nayo iliwaponyoka kwa kumfanya mwanadamu kuwa Mungu. Na kama miujiza ya zamani ielezwe ambayo sasa ni kama visa tu, hapo kwanza kila mkana anaweza kusema kuwa Mungu Ajua uhakika wake ukoje! kiasi gani imetiliwa chumvi, kwani hakuna shaka yoyote kwamba kutia chumvi ilikuwa kawaida ya waandishi wa Injili. Katika Injili moja mna mstari huu kuwa Masihi alifanya kazi nyingi sana ambazo kama zingeandikwa, dunia isingetosha? Sasa hebu angalieni kuwa bila kuandikwa dunia ilitosha kwazo lakini

zikiandikwa dunia haitatosha kwazo! Ni aina ya gani falsafa hiyo na ni mantiki gani!! Je, kuna yeyote anayeweza kuielewa?

Mbali na hii, miujiza ya Hadhrat Masihi[as] haikuizidi miujiza ya nabii Musa[as] Na ishara za nabii Eliya zikilinganishwa na ishara za Masihi, hapo miujiza ya Eliya zitakuwa na uzito zaidi. Hivyo, kama kwa miujiza mtu anaweza kuwa Mungu, basi watawa wote hawa wanastahiki kuwa miungu. Na jambo hili kwamba Yesu amejieleza kuwa yu mwana wa Mungu au katika kitabu fulani ameitwa mwana, basi haifai kuhakikisha uungu wake kutokana na maandishi ya namna hiyo.

Ndani ya Biblia watu wengi wameitwa wana wa Mungu, bali wengine miungu pia, basi hakuna sababu ya kumchagua Yesu peke yake. Na hata kama mtu yeyote minghairi ya Masihi asingepewa lakabu ya Mungu au mwana wa Mungu, hata hivyo si busara kuyachukulia maneno ya aina hiyo katika maana halisi, kwani katika neno la Mungu kuna istiara nyingi sana. Lakini kama sawa na Biblia wengine pia wanashirikiana na Masihi katika kuitwa mwana wa Mungu, kwa nini washiriki hao wengine nao wananyimwa heshima hiyo?

Ilmuradi, kuitegemea sera hiyo kwa kupata wokovu si sahihi; na kuepukana na dhambi hakuhusiani na sera hiyo hata kidogo; bali kujiua kwenyewe ili kuwaokoa wengine ni dhambi. Na mimi naweza kusema kwa kuapa kwa jina la Mwenyezi Mungu kuwa Yesu hakukubali kuwambwa juu ya msalaba kwa ridhaa yake mwenyewe, bali Mayahudi wakorofi walimfanyia walivyotaka. Na Yesu usiku kucha akaomba dua ndani ya bustani ili aepukane na kifo

cha msalabani, machozi yake yakatiririka. Ndipo Mwenyezi Mungu Akapokea maombi yake kwa sababu ya utawa wake na Akamwokoa katika kifo cha msalaba kama ilivyoandikwa ndani ya Injili. Basi tuhuma hii ni ya namna gani kuwa Yesu alijiua kwa ridhaa yake mwenyewe! Aidha, haiingii akilini kwamba bwana Zaidi ajipige jiwe kichwani na bwana Bakari apone maumivu yake ya kichwani. Naam, sisi tunakubali kuwa Hadhrat Masihi[as] alikuwa nabii mmoja na alikuwa miongoni mwa waja wakamilifu Aliowatakasa Mwenyezi Mungu kwa mkono Wake, lakini kwa sababu ya maneno yaliyomo katika vitabu kumhusu yeye au manabi wengine hatuwezi kumfanya yeye au nabii mwingine yeyote kuwa Mungu. Mimi ni mzoefu wa mambo haya, na kunihusu mimi katika wahyi mtakatifu wa Mungu kuna maneno ya heshima na staha nisiyoyaona ndani ya Injili kumhusu Hadhrat Masihi. Sasa, je, mimi naweza kusema kuwa kweli mimi ni Mungu au mwana wa Mungu? Ama mafundisho ya Injili, basi maoni yangu ni kwamba mafundisho kamili huwa yale yanayolea nguvu zote za mwanadamu, yasiyotilia mkazo wote upande mmoja tu. Nasema kweli kweli kuwa mafundisho makamilifu nimeyakuta ndani ya Kurani Tukufu tu; hiyo inaendelea kutunza haki na hekima katika kila jambo. Kwa mfano, imesemwa ndani ya Injili kuwa ukipigwa kofi shavu moja umgeuzie na la pili pia, lakini Kurani Tukufu inatufundisha kuwa fundisho hili halihusikani na hali zote na mahali pote, bali yafaa kuzingatia hali yenyewe kwamba inahitaji subira au kisasi, msamaha au adhabu. Sasa ni dhahiri kuwa mafundisho haya ya Kurani ndiyo makamilifu na bila kuyafuata mwendeleo wa maisha ya binadamu unaangamia na

utaratibu wa dunia unavurugika. Kadhalika imesemwa ndani ya Injili kuwa usimtazame mwanamke asiyehusika kwa tamaa. Lakini ndani ya Kurani Tukufu imo kwamba usiwe na mazoea ya kutazama wanawake wasiohusika kwa tamaa wala bila tamaa, kwani hapo ni mahali pa kujikwaa. Yafaa kuwa wakati wa mahitaji macho yako yawe karibu yamefumbwa, uangalie kwa kuinamisha macho, na ujizuie kuona kwa macho wazi sana. Kwani, hiyo ndiyo njia ya kulinda utakaso wa moyo. Pengine madhehebu ya kiupinzani ya zama hizi yatayapinga amri hii, kwani ndiyo shauku mpya mpya ya uhuru. Lakini tajiriba inabainisha wazi kwamba mafundisho haya ndiyo yaliyo sahihi. Enyi marafiki! matokeo ya kuchanganyikana na kutongozeana ovyo kamwe hayawi mazuri. Kwa mfano, katika hali ambapo mwanamume hajatakasika katika tamaa za nafsi na mwanamke kijana naye hajatakasika katika tamaa za nafsi, kuwapa hawa wawili mwanya wa kukutana na kutongozeana kwa uhuru ni sawa na kuwasukumia ndani ya shimo kwa mikono yenu. Kadhalika imesemwa ndani ya Injili kuwa talaka haiwezi kutolewa bila zinaa kutendeka, lakini Kurani Tukufu inaruhusu kutoa talaka kama kwa mfano mume na mke wamekuwa maadui wakubwa na kila mmoja akahatarisha maisha ya mwenzake, au mke hakufanya zinaa lakini amezalisha mazingira ya kizinaa, au amepata maradhi ambayo ndiyo maangamio kwa mume wakikutana kimwili, au ikapatikana sababu yoyote nyingine ambayo machoni mwa mume ndiyo chanzo cha kutoa talaka. Katika hali zote hizo mume hatalaumiwa endapo atatoa talaka.

Sasa tunarejea kwenye madhumuni yetu na tunasema kuwa kumbukeni kabisa kwamba Wakristo hawana njia yoyote ya kweli ya kupata wokovu na ya kuepukana na dhambi, kwani hakuna maana yoyote ya wokovu ila kwamba hali ya mtu iwe kuwa asipate kujasiri kutenda dhambi, na yaongezeke mapenzi ya Mwenyezi Mungu kiasi hiki kwamba mapenzi ya matamanio ya kimwili yasiweze kuyashinda. Na ni dhahiri kuwa hali hii haiwezi kupatikana pasipo utambuzi kamili. Sasa tunapoisoma Kurani Tukufu, humo tunazikuta wazi wazi njia ambazo kwazo twaweza kupata utambuzi kamili wa Mwenyezi Mungu na kisha kuweza kuepukana na dhambi kwa kutawaliwa na hofu. Kwani tunashuhudia kuwa kwa kufuata huku maongezi na Mwenyezi Mungu hupatikana, na ishara za kimbinguni hudhihirika, na mwanadamu hupata elimu za mambo ya ghaibu kutoka kwa Mungu, na uhusiano madhubuti naye huzalika, na moyo hupata uharara ili kumlaki Mungu, naye humtanguliza Yeye juu ya kila kitu, na yakikubaliwa maombi hupewa habari, na mto wa utambuzi wa Mungu huanza kutiririka ambao unamwepusha na dhamabi. Na tunapoielekea Injili tunaikuta njia moja tu isiyoingia akilini ya kuepukana na dhambi ambayo haihusiani kabisa na kuondoa dhambi. Ni ajabu kwamba  Bwana Yesu alionyesha udhaifu mwingi wa kibinadamu, na haikudhihirika kutoka kwake nguvu maalum ya Kiungu ambayo ingemtofautisha na wengine, hata hivyo  machoni mwa Wakristo akatambuliwa kuwa Mungu.

Sasa kwa muhtasari tunaliangalia dhehebu la Ariya kwamba katika dhehebu lao imewekwa njia ipi ya kuepukana na dhambi. Basi ibainike kuwa kitabu

kitakatifu cha Veda cha Waariya kimekataa kwa siku zijazo kuwepo kwa maongezi ya Mwenyezi Mungu na ishara za kimbingu. Hivyo, basi, kutafuta utulivu kamili katika Veda kuwa mtu apate kusikia sauti ya Mungu kwamba 'Nipo', na Mungu ajibu baada ya kusikia maombi, na kwa njia ya ishara Aonyeshe uso Wake, ni juhudi ya bure na utafutaji usioweza kufanikiwa, bali kwao kazi hii yote ni jambo lisilowezekana. Lakini ni wazi kabisa kuwa kukipenda au kukihofu kitu hakuwezekani bila kukiona na kukitambua kikamilifu. Na kwa kuangalia tu vitu vilivyotengenezwa, utambuzi uliokamilika hauwezi kupatikana. Ndiyo maana miongoni mwa waifuatao akili tupu, maelfu ya madaharia na wamkanao Mungu wanapatikana; bali wale watu wanaofikia kilele cha falsafa, hao ndio watakiwa kuitwa madaharia kikamilifu. Na tumekwisha eleza sasa hivi kuwa akili timamu inaweza kufaa mpaka kiasi hiki tu kuwa kwa kuangalia vitu vilivyotengenezwa – sharti isiwe na udaharia ndani mwake – inaweza kupendekeza kuwa Mwumbaji wa vitu hivyo Anapaswa Awepo, siyo kwamba Mwumbaji yupo pia kwa kweli. Na tena akili nayo inaweza kuingiliwa na dhana kwamba yawezekana utaratibu huu wa dunia unaedelea wenyewe, na kwa kiasili baadhi ya vitu vimeviumba vingine. Basi akili haiwezi kufikisha kwenye yakini kamilifu inayoitwa utambuzi kamili ambao ni kama kumuona Mungu, na ambao kwao hofu na upendo kikamilifu huzalika na kisha kutokana na moto wa hofu na upendo dhambi ya kila aina huunguzwa na tamaa za nafsi hujifia na baada ya kupatikana badiliko la kiroho lenye nuru unyonge wote wa ndani na ucafu wote wa dhambi hutoweka. Lakini kwa kuwa wanadamu wengi

hawajali utakaso huu mkamilifu unaoondoa kabisa doa la dhambi, kwa hiyo watu wengi wasiposikia haja yake hawajishughulishi kuutafuta; bali kinyume chake kwa sababu ya kujaa chuki, hudhihirisha upinzani na wanakuwa tayari kupigana. Madhehebu ya Waariya ni ya kusikitisha sana. Hao wameisha kata tamaa kabisa katika kupata njia ya kweli ya utambuzi kamili na wala hawana hata mbinu za kiakili mkononi mwao, kwani wanaamini kila chembe ya ulimwengu ni ya tangu azali, ipo tu yenyewe wala haikutengenezwa na mkono wa yeyote, na roho zote pamoja na nguvu zao zote nazo ni za tangu azali ambazo hazina Mwumbaji wao. Basi kuna dalili gani iliyobaki mkononi mwao kuthibitisha kuwepo kwa Mungu? Na wakisema kuwa kazi ya Mungu ni kuunganisha chembe za ulimwengu na kuingiza roho ndani yao, na hiyo ndiyo dalili ya kuwepo kwake, basi wazo hili halitakuwa sahihi. Maana kama roho na chembe zenyewe zina uwezo wote na zinajisimamia tangu azali na zenyewe ni miungu wao, je, haziwezi zenyewe kuungana na kutengana? Hakuna yeyote atakayekubali ya kwamba juu ya chembe zote kutokumhitaji mwingine kwa kuwepo kwao, na juu ya roho zote kutomhitaji yeyote mwingine kwa kuwepo kwao na nguvu zao, hizo zote zinamhitaji mwingine kwa kuungana na kutengana kwao. Hii ndiyo itikadi iliyo windo rahisi kwa wasiomwamini Mungu. Na kwa hiyo Mwariya anaweza kuingia haraka sana katika udaharia, na mtu mjanaja asiyemwamini Mungu anaweza kumnasa kwa urahisi sana. Mimi ninasikitika sana na kuwahurumia pia kwamba Waariya wamekosea sana katika pande zote mbili za sheria. Yaani, kumhusu Mungu wamekuwa na itikadi kuwa Yeye si chanzo

cha viumbe vyote wala si chemchem ya upaji wote, bali eti chembe zote pamoja na nguvu zao zote, na roho zote pamoja na nguvu zao zote zipo tu zenyenwe, na tabia zao za asili zimenyimwa baraka Zake. Basi, fikirini wenyewe kwamba kuna haja gani ya Mungu, na kwa nini Yeye Anastahiki kuabudiwa, na kwa nini Anaitwa Mweza Halisi, na namna gani na kwa njia gani Ametambuliwa. Je, yuko anayeweza kujibu swali hili? Laiti huruma yetu ingeathiri moyo wowote! Laiti mtu yeyote angekaa pembeni peke yake na ayafikirie maneno haya!! Ee Mungu Mweza! wahurumie watu hawa ambao ni jirani zetu tangu zamani; kutoka miongoni mwao waelekeze wengi mioyo yao kwenye haki, kwani Unao uwezo wote. Amin. Upande huu ndio kumhusu Mungu ambapo Mwumbaji wa pekee Amenyanganywa haki. Na upande wa pili ambao dini ya Kiariya inaweka mbele yetu kuhusu viumbe, sehemu yake moja ni *Tanasukh*, yaani roho kwa vipindi mbalimbali kurejea duniani mara kwa mara katika umbo tofauti. Katika itikadi hii jambo la kwanza la ajabu linaloshangaza ni kwamba juu ya madai ya kutumia akili imefikiriwa kuwa Mungu ni Mwenye moyo mgumu kiasi hiki kuwa kwa dhambi moja Anaendelea kuadhibu kwa mamilioni bali mabilioni ya miaka, ilhali Anajua kuwa Yeye siye Mwumbaji wao, na hana haki yoyote juu yao, sembuse kutia katika vipindi mbalimbali katika sura tofauti na kuwaudhi. Kwa nini haadhibu kwa miaka michache kama serikali ya wanadamu? Ni wazi kuwa kutoa adhabu kwa muda mrefu sana kuna sharti kwamba kuwe na haki pia juu ya waadhibiwa. Lakini katika hali ambapo chembe zote na roho zote zipo tu zenyewe, Yeye Hakuzifanyia hisani yoyote, isipokuwa tu Akazitia katika vipindi mbalimbali na

kuleta duniani mara kwa mara kwa sura tofauti kwa kuwapa adhabu, basi Ana haki gani ya kutoa adhabu ndefu? Hebu angalieni! ndani ya Islam ingawa Mungu Anasema Mimi ndimi Mwumbaji wa kila chembe na kila roho, na nguvu zao zote ni kwa baraka inayotoka kwangu na zimeumbwa kwa mkono Wangu na zinaishi kwa kunitegemea Mimi, hata hivyo Anasema ndani ya Kurani Tukufu:

اِلَّا مَا شَآءَ رَبُّكَ ؕ اِنَّ رَبَّكَ فَعَّالٌ لِّمَا يُرِيْدُ ○ [30]

Yaani, watu wa motoni watakaa humo milele. Lakini hapa 'milele' siyo maana yake kama Mungu Akaavyo milele, bali yamaanisha tu muda mrefu. Kisha rehema ya Mungu itakuja saidia, kwani Yu Mweza, Hufanya Apendavyo. Na kuna Hadithi ya Seyyidna na Maulana Mtume Mtukufu[saw] inayofafanua aya hii, nayo ndiyo:

يَأْتِىْ عَلٰى جَهَنَّمَ زَمَانٌ لَيْسَ فِيْهَا اَحَدٌ وَ نَسِيْمُ الصَّبَا تُحَرِّكُ اَبْوَابَهَا

Yaani, zama zitakuja juu ya jahanamu ambapo hamtabakia yeyote ndani yake na upepo wa mashariki utatikisisha milango yake. Lakini ni masikitiko kwamba watu hao wanamhesabu Mwenyezi Mungu kuwa mwenye kasirani na chuki ambaye hasira zake kamwe haiondoki, hata baada ya kutia katika vipindi mbalimbali kwa kuleta duniani mara kwa mara katika sura tofauti hasamehe dhambi.

Na hoja hii haitolewi dhidi ya Waariya tu, Wakristo pia wana itikadi kuwa adhabu ya dhambi moja ni kukaa katika jahanamu milele ambayo haina kikomo, na papo hapo wana itikadi hii pia kuwa Mungu ni

[30] Huud: 108

Mwumbaji wa kila kitu. Basi ikiwa Mungu Mwenyewe ndiye Mwumbaji wa roho za watu na nguvu zao zote, naye ndiye Aliyeziwekea udhaifu kadha baadhi ya tabia za asili hata kwamba zinapata kutenda dhambi, na zinafanya kazi mfano wa saa mpaka hapo alipoipangia mwundaji wa saa, hivyo lazima zinastahiki huruma kiasi fulani, kwani makosa yao na udhaifu wao sio waliojipangia wao wenyewe, bali Mwumba naye Yumo katika habari hii Aliyewafanya dhaifu. Na ni uadilifu gani huu kuwa Alimwekea mwanaye siku tatu tu kwa kumwadhibu, lakini wengine akawapangia adhabu ya milele isiyo na kikomo kabisa, na Akataka waendelee kuungua ndani ya tanuri la jahanamu milele hata milele. Je, ilimpasa Mrehemevu Mkarimu kufanya hivi? Bali ilimpasa kumwadhibu mwanaye zaidi, maana kwa sababu ya nguvu za kiungu angeweza kustahimili adhabu nyingi zaidi, kwani yu mwana wa Mungu, nguvu yake inawezaje kuwa sawa na nguvu ya wengine ambao ni viumbe maskini na dhaifu. Hivyo basi, Wakristo na Waariya wametegwa katika mtego wa hoja moja, na pamoja nao wako baadhi ya Waislamu wajinga pia. Lakini katika kudanganyika kwa Waislamu, neno la Mungu halimo. Mungu Alikwisha eleza kwa uwazi kuwa hili ni kosa lao wenyewe; na kosa hili ni kama lile la kusema kuwa Hadhrat Isa[as] yu hai mpaka sasa, na wanamkalisha kwenye mbingu wa pili ilhali katika Kurani Tukufu imeandikwa wazi kuwa Hadhrat Isa[as] ameisha fariki muda mrefu uliopita na amekwisha ungana na roho za waliopita. Lakini kinyume cha kitabu cha Mungu bado wanasubiri ujaji wake wa mara ya pili. Tunarudia maudhui yetu na tunasema kuwa jiha ya pili ya kubatilisha imani ya *Tanasukh* ni kuwa hii ni

kinyume cha utakaso wa kweli. Maana sisi kila siku tunaona mama wa fulani amefariki, au dada ya fulani au mjukuu wa kike wa fulani amekufa, sasa kuna dalili gani kuwa wenye itikadi hii hawatafanya kosa la kumwoa yule aliyeharamishwa na kitabu cha Veda. Naam, kama wakati wa kuzaliwa kila mtoto awe na urodha ambamo iwe imeelezwa kwamba mzaliwa huyu katika awamu iliyopita alikuwa mtoto wa mtu fulani, hapo wangeliweza kuepukana na ndoa isiyo halali. Lakini Mungu hakufanya hivyo; kana kwamba Mwenyewe Alitaka kueneza njia ya haramu. Aidha, sisi hatuelewi kuwa kuna faida gani ya kuwaingiza katika mfuatano wa kuzaliwa kwa sura mbalimbali. Kama wokovu wote unategemea utambuzi wa Mungu, basi ilipasa kuwa kila mtoto anayezaliwa mara ya pili, mkusanyiko wa elemu na utambuzi wake wa zamani usingelipotea. Lakini ni dhahiri kuwa kila mtoto anayezaliwa huja duniani mikono mitupu, na kama mtu mpotovu na mbadhirifu akiangamiza akiba ya awali, hubakia kama mtu maskini asiye na kitu. Na hata kama alipata kusoma Veda Takatifu mara elfu, hakumbuki hata ukurasa mmoja wa Veda. Hapo katika mfuatano wa kuzaliwa kwa sura tofauti, njia ya wokovu haionekani; kwani mkusanyiko wa elimu na maarifa unaokusanywa katika kila kipindi cha kuzaliwa kwa taabu na shida sana unaendelea kuangamia pale pale; hautahifadhika wala wokovu hautapatikana. Kwanza, kwa mujibu wa sheria za Waariya, wokovu ulikuwa wa muda tu, kisha juu yake kuna shida hii kwamba mtaji wa wokovu, yaani elimu, haupati kukusanyika. Kama hii siyo bahati mbaya ya roho, ni nini tena?

Jambo la pili lilio kinyume cha utakaso wa viumbe ambalo limo katika itikadi za Waariya ni masaala ya "Neoga". Masaala haya sisemi yamo katika kitabu kitakatifu cha Veda; bali moyo wangu hutetemeka kwa kufikiria kuwa mimi niyanasibishe mambo haya kwa Veda. Kadiri ninavyojua na dhamiri niliyo nayo, nina yakini kwamba tabia ya asili ya mtu haitakubali kwamba ili kupata tu mtoto yeye amfanye mkewe safi mwenye ukoo mzuri na mwenye heshima kulala na mwanamume mwingine ilhali yu bado mke wa mumewe na anaitwa mke wake. Wala sipendi kwamba mke mwenywe awe tayari kutenda kitendo cha namna hii ilhali mumewe yupo hai. Si binadamu tu, hata baadhi ya wanyama pia wana ghera hii ya kwamba hawavumilii majike yao kufanyiwa hivyo. Hapa sitaki kufanya majadiliano yoyote, ila kwa adabu na unyenyekevu ninawaomba Waariya kuwa kama wakiacha itikadi hii, itakuwa bora. Mapema nchi hii imerudi nyuma katika utakaso wa kweli, kisha kama mambo ya aina hii yakiwa desturi baina ya wanawake na wanaume, haijulikani nchi hii itakuwa na mwisho gani. Pamoja na hii najasiri kusema ya kwamba ingawa Waariya katika siku hizi hata wanawachukia Waislamu namna gani, na hata wanazibeza itikadi za dini ya Kiislamu vilivyo, lakini kwa jina la Mungu, desturi ya wanawake kujifunika shungi wasiiache kabisa, kwani katika kuiacha desturi hii kuna maovu mengi yatakayojulikana baadaye. Jambo hili kila mtu fahamivu anaweza kulielewa kwamba wanadamu wengi wanatawaliwa na nafsi inayoamrisha maovu na wameshikwa na nafsi zao kiasi hiki kwamba wakati wa harara ya tamaa ya nafsi hawakumbuki adhabu ya Mwenyezi Mungu, hawajizuii kutazama wanawake vijana na wazuri, na

kadhalika wako wanawake wengi ambao wanawatazama wanaume wasiohusika kwa nia mbaya. Na juu kuwa katika hali hii mbaya wanawake wanaume wakipewa uhuru bila shaka matokeo yake yatakuwa yale yanayoonekana katika baadhi ya sehemu za Ulaya. Naam, wakati ambapo watu hawa watatakasika kweli mioyo yao na tamaa ya nafsi yao itapotea, na roho ya kishetani itaondoka na machoni mwao itazalika hofu ya Mungu, na utukufu wa Mungu utaimarika mioyoni mwao, nao watapata mabadiliko mema na watavaa joho la ucha-Mungu; hapo wafanye watakalo, maana wakati huo watakuwa matowashi wa mkono wa Mungu, kana kwamba hao sio wanaume, na macho yao yatakuwa mapofu yasiweze kuwatazama wanawake wageni kwa nia mbaya au kuweza kuleta wazo baya moyoni. Lakini enyi wapenzi! Mungu Mwenyewe Awafunulieni mioyoni mwenu, huu sio wakati wa kufanya hivyo; na kama mkifanya hivyo mtakuwa mnasambaza mbegu mbaya ya sumu katika kaumu. Zama hizi ni za hatari sana kwamba hata kama katika zama nyingine kusingekuweko na desturi ya kufunika shungi, katika zama hizi lazima ingekuwepo, maana hizi ni zama za mwisho na uovu, ufuska na upujufu na unywaji pombe vimepamba moto ardhini, na mawazo ya udaharia yanapata kuingia nyoyoni, na adhma ya amri za Mwenyezi Mungu imetoweka mioyoni. Midomo hutamka mambo yote, hotuba nazo hutolewa zilizojaa mantiki na falsafa, lakini mioyo ni mitupu, haina utawa. Katika hali kama hii haifai kabisa kuacha mbuzi zenu maskini ndani ya pori la mbwa mwitu.

Enyi marafiki, hivi sasa tauni inapiga hodi. Na kadiri nilivyojulishwa na Mwenyezi Mungu, sehemu kubwa

ingali bado. Ni siku za hatari sana. Haijulikani kuwa mpaka mwezi Mei ujao nani atabaki hai na nani atakufa, na nyumba gani itafikiwa na balaa na gani itakingwa. Basi, amkeni, mkatubu na kumridhisha Bwana Wenu kwa matendo mema. Na kumbukeni kuwa adhabu ya makosa ya itikadi itatolewa baada ya kufa, na uamuzi juu ya kuwa Mhindu, Mkristo au Mwislamu utatolewa siku ya kiama. Lakini mtu anayepita kiasi katika dhulma, uhalifu, ufasiki na upujufu, huadhibiwa hapa hapa, hapo yeye hawezi katu kuikimbia adhabu ya Mungu. Basi, Mridhisheni haraka Mungu wenu, na kabla ya kuja siku ile yenye kutisha, yaani siku ya nguvu ya tauni iliyotolewa habari zake na manabii, fanyeni suluhu na Mungu. Yu Mkarimu, kwa toba ya mara moja iliyojaa unyeyekevu mkubwa, Yeye huweza kusamehe madhambi ya miaka sabini. Msiseme kuwa toba haikubaliwi. Kumbukeni, kamwe hamwezi kusalimika kwa matendo yenu, bali daima fadhili ya Mungu ndiyo husalimisha siyo matendo. Ewe Mungu Mkarimu na Mrehemevu, tujalie sote fadhili zako, kwani tu watumishi wako na tumeangukia kizingiti chako. Amin.

# SEHEMU YA PILI YA HOTUBA

Enyi wasikilizaji waheshimiwa! sasa mimi nitawaelezeni machache kuhusu madai yangu niliyotangaza nchini humu. Jambo hili limethibitika kwa akili na maandiko kuwa giza la dhambi linapotanda duniani, na uovu wa kila namna na uasherati unapoenea ardhini, na ucha Mungu unapopungua, na upepo wenye sumu unapoanza ya kuvuma baada ya ardhi kunajisika kwa madhambi na mapenzi ya Mwenyezi Mungu kupoa, hapo huruma ya Mungu hutaka kuhuisha ardhi mara nyingine tena. Kama vile mnavyoishuhudia misimu ya kimwili siku zote inabadilika badilika ─ kuna msimu mmoja wa kharifu[31] ambapo maua ya miti, matunda na majani hunyauka na kupukutika, miti hupata sura mbaya kama mgonjwa wa kifua kikuu anavyokonda sana na kupungukiwa kabisa damu na alama za mauti hudhihirika usoni, au sawa na ugonjwa wa ukoma uliokomaa na kuanza husababisha viungu kukatika katika; kisha miti inafikiwa na kipindi cha pili kinachoitwa msimu wa rabiu;[32] katika msimu huu sura za miti hupata hali nyingine, matunda na maua na majani mazuri na mabichi hudhihirika ─ ndivyo ilivyo hali ya mwanadamu kuwa giza na mwanga humfikia kwa awamu. Katika karne fulani huondokewa na uzuri wa ukamilifu wa kibinadamu kama msimu wa kharifu, na katika muda mwingine

[31] Kharifu ni msimu wa kunyauka majani ya miti na kupukutika, unaoitwa Autum kwa Kiingereza. (mfasiri)

[32] Rabiu ni msimu wa kuchipua na kuchanua – Spring kwa Kiingereza. (mfasiri)

upepo unawapepea kutoka mbinguni unaowaletea msimu wa rabiu mioyoni. Tangu ulimwengu uumbwe, misimu hiyo miwili ndiyo inayoambatana na mwanadamu. Basi zama hizi tulizonazo hivi sasa ni mwanzo tu wa zama za rabiu. Katika Panjab zama za kharifu zilikuwa kali sana wakati Masingasinga walitawala nchi hii, maana elimu ilitoweka na ujinga ulienea nchini na vitabu vya dini villipotea kabisa, pengine vingeweza kupatikana katika ukoo mkubwa na maarufu tu. Baada ya hapo zikaja zama za serikali ya Kiingreza. Zama hizi ni za amani sana, na ukweli wenyewe ni kwamba hata tukizichukulia zama za michana ya serikali ya Masingasinga kwa amani na raha kuwa sawa na mausiku ya zama za serikali ya Waingereza, itakuwa ni dhuluma na kinyume cha hali ilivyo. Zama hizi ni mkusanyiko wa baraka za kimwili na kiroho, na baraka zijazo ziko wazi kutokana na mwanzo wa rabiu yake. Lakini zama hizi mithili ya mnyama wa ajabu zina vinywa vingi, baadhi ya vinywa vinatisha kwa sababu ya kuwa kinyume cha utambuzi halisi wa Mungu na ukweli, na baadhi ya vinywa vina baraka nyingi na vinasaidia sana ukweli. Lakini hakuna shaka kuwa serikali ya Kiingereza imezipa sana maendeleo elimu za aina mbalimbali nchini humu. Na zimepatikana njia rahisi za kuchapisha na kueneza vitabu, ambazo mfano wake haupatikani katika zama zilizopita. Na maelfu ya maktaba zilizokuwa zimefichikana nchini humu nazo zimedhihirika, na katika siku chache hali ya zama ikabadilika kielimu kana kwamba taifa jipya limezaliwa. Haya yote yalitokea, lakini amali ziliendelea kutoweka siku hadi siku, na ndani kwa ndani udaharia ukaanza kukua. Hakuna shaka katika hisani ya serikali ya Kiingereza, imefanya hisani

nyingi kwa raia zake na kufanya uadilifu, na kuimarisha amani hapa na pale hata kwamba hakuna mfano wake katika serikali zingine. Lakini ule uhuru waliopewa raia ili amani ipatikane kikamilifu, watu wengi hawakuweza kuutumia vizuri. Walitakiwa kumshukuru Mungu na serikali kwa sababu hiyo; lakini badala ya shukurani, imezidi sana katika mioyo mingi kughafilika, kufuata mambo ya dunia na kutaka dunia na kutojali, kana kwamba imefikiriwa kuwa dunia tu ndiyo mahali petu pa kukaa sikuzote. Kana kwamba hakuna juu yetu hisani ya yeyote, wala hakuna juu yetu utawala wa yeyote. Na kama ilivyo kawaida, dhambi nyingi huzalika katika hali ya amani.

Basi kwa kanuni hiyo ya asili idadi ya dhambi pia iliendelea kuongezeka. Hivyo, kutokana na ugumu wa mioyo na hali ya kughafilika, hali ya sasa ya nchi hii imekuwa hatari sana. Watu majahili na wenye shari ambao ni kama hayawani wamejiingiza katika uhalifu mchafu kama vile wizi wa kuingia nyumbani usiku, uzinzi na kuua pasipo haki  na kadhalika. Na watu wengine sawa na tabia na tamaa ya nafsi yao wanaendelea kutenda madhambi mengine mbalimbali. Vilabu vya pombe vyaendewa kuliko maduka mengine; na kazi za maovu mengine pia zinasonga mbele siku hadi siku; nyumba za ibada zipo kwa kutimiza kwaida tu. Ilmuradi madhambi yanafanyika ardhini kwa nguvu sana. Na tamaa za nafsi za watu wengi zimechemka sana kwa sababu ya amani kamili na starehe kamilifu, kiasi hiki kwamba kama boma la kuzuia maji ya mto unaopita kasi kwa nguvu likibomoka, basi katika usiku mmoja tu huangamiza vijiji vyote vya kandokando yake. Na hakuna shaka kuwa dunia imegubikwa na giza totoro

na umefika wakati ambapo ama Mungu Alete mwanga au Aiangamize dunia. Lakini bado imebakia miaka elfu moja kwa dunia hii kuangamia. Na kwa mapambo, raha na starehe za dunia, vitu vipya vipya vimetengenezwa duniani; mabadiliko haya pia yanathibitisha kwa uwazi kuwa jinsi Mwenyezi Mungu Alivyorekebisha hali ya kimwili, ndivyo anavyotaka upatikane urekebisho na maendeleo ya kiroho kwa ajili ya binadamu. Kwani hali ya kiroho ya binadamu imerudi nyuma zaidi kuliko hali ya kimwili, na imefikia mahali pa hatari ambapo mwanadamu anaweza kughadhibikiwa na Mungu. Uchu wa kila dhambi umezidi sana na nguvu za kiroho zimefifia kabisa na nuru ya imani imezimika. Sasa akili timamu inakubali kwa uwazi haja ya kwamba katika hali ya giza kuenea, mwanga unatakiwa upatikane kutoka mbinguni, kwani kama ambavyo kuondoka kidhahiri giza la ardhini kulitegemea tangu zamani mwanga wa mbinguni kufika ardhini ndivyo hivyo kiroho pia mwanga huu unashuka kutoka mbinguni tu na kuing’arisha mioyo. Tangu Mungu Alipomwumba mwanadamu, kanuni yake ya asili imeshuhudiwa kuwa ili kuleta umoja kati ya wanadamu, Yeye wakati wa haja humtupia mtu mmoja miongoni mwao nuru ya utambuzi wake kamili na Humpa heshima ya kuongea naye na Humjalia mapenzi yake makamilifu na Humpatia busara kamili ya njia yake aliyoipenda, na Humtilia jazba moyoni mwake ili awavutie na wengine pia kwenye nuru, busara na upendo aliopewa yeye. Na kwa njia hii watu wengine wakijenga uhusiano naye na wakihesabiwa kuwa ndani ya dhati yake na kupata sehemu ya utambuzi wake wanaepukana na dhambi na kupiga hatua katika utakaso na ucha Mungu.

Kutokana na kanuni hiyo ya zamani, Mungu kwa njia ya manabii wake watakatifu Ametoa habari kwamba miaka elfu sita itakapokaribia kwisha tangu wakati wa Adam, giza kubwa litaenea ardhini na mafuriko ya dhambi yataanza kutiririka kwa nguvu sana, na mapenzi ya Mungu yatapungua mno mioyoni na yatakuwa kama yamepotea, ndipo Mungu kutoka mbinguni, bila kutumia njia za ardhini, Atampulizia mtu mmoja, mfano wa Adamu, roho ya ukweli, mapenzi na ya utambuzi wake, naye ataitwa Masihi pia, kwani Mungu kwa mkono Wake Atampaka uturi wa mapenzi yake Mwenyewe, na yule Masihi wa ahadi ambaye kwa maneno mengine ametajwa ndani ya vitabu vya Mungu kuwa Masihi Aliyeahidiwa atasimamishwa dhidi ya shetani, na hii itakuwa vita ya mwisho baina ya jeshi la kishetani na Masihi. Siku hiyo shetani atakuja pamoja na nguvu zake zote, dhuria zake zote na hila zake zote akijitayarisha kwa ajili ya vita hii ya kiroho.

Na vita baina ya shari na heri huenda ikawa haijapiganwa hapo kabla kama itakvyokuwa siku hiyo, kwani siku hiyo hila za shetani na elimu za kishetani zitakuwa zimefika kileleni na njia zote anazoweza shetani kutumia kuwapoteza watu, njia zote hizo zitapatikana siku ile. Ndipo baada ya vita kali iliyo vita ya kiroho, Masihi wa Mungu atapata ushindi na nguvu za kishetani zitaangamia, na kwa muda fulani jalali ya Mungu na adhma, utakaso na umoja wa Mungu vitaendelea kuenea duniani, na muda huo ni miaka elfu moja kamili unaoitwa siku ya saba, baada ya hapo dunia itakwisha. Basi yule Masihi ndiye mimi, yeyote akitaka akubali. Hapa baadhi ya madhehebu yanayokataa kuwepo kwa

shetani watashangaa kuwa shetani ni kitu gani? Wao wakumbuke kuwa mivutnao miwili kwa awamu daima inaambatana pamoja na moyo wa mwanadamu, mvutano mmoja wa heri, na mvutano mwingine wa shari. Ule mvutnao wa heri, sheria ya Islam inaunasibisha kwa malaika, na mvutano wa shari unanasibishwa na sheria ya Kiislam kwa shetani. Ndiyo kusema kwamba katika tabia ya asili ya mwanadamu mna mivutnao miwili; pengine mwanadamu huelekea kwenye wema na mara nyingine kwenye ubaya. Nafikiri katika mkutano huu pengine wako watu wengi pia ambao watakana kauli yangu hii kwamba mimi ni Masihi Mau'udi na ninajaaliwa heshima ya kuongea na Mungu, na wataniangalia kwa dharau. Lakini mimi nawaona wana udhuru, kwani tangu mwanzo inaendelea kuwa hivi kwamba wajumbe na mitume wa Mungu kwanza wanalazimika kusikia maneno ya kuumiza mioyo. Nabii havunjiwi heshima ila katika zama zake za mwanzo. Yule Nabii na Mjumbe na mwenye kuleta kitabu na mwenye sheria ambaye sisi sote tunaona fahari kuwa katika umati wake, na ambaye sheria yake ndiyo mwisho wa sheria zote, hebu iangalieni historia ya maisha yake kwamba kwa muda wa miaka kumi na mitatu katika Makka katika hali ya upweke na umaskini na bila msaada wowote aliteswa namna gani na wakataaji wa madai yake na akaendelea kuwa shabaha ya dharau na mzaha na dhihaka; hatimaye akafukuzwa katika Makka kwa kudhulumiwa sana na uonevu. Nani alijua kuwa yeye hatimaye atafanywa Imam na Kiongozi wa mamilioni ya watu! Basi, hii ndiyo suna ya Mungu kuwa wateule wa Mungu mwanzoni hufikiriwa kuwa hakiri na dhalili; na ni watu wachache tu wanaoweza kuwatambua

mwanzoni wanaotumwa na Mungu. Ni lazima wapate kuteswa kwa mikono ya wajinga, na maneno ya namna namna yaongelewe juu yao, na wachekewe, wadhihakiwe na watukanwe mpaka ufike wakati ambapo Mungu Atafungua mioyo kuwakubali. Hayo ndiyo madai yangu niliyoeleza, lakini kazi Aliyonituma Mungu kuifanya ni hii kwamba uchafuzi uliotokea katika uhusiano wa viumbe waliokuwa na Mungu, niuondolee mbali huo uchafuzi na kuimarisha mara nyingine uhusiano wa upendo na ikhlasi; na kwa kudhihirisha ukweli nikimaliza vita vya kidini niweke msingi wa suluhu; na zile kweli za kidini zlizofichikana kwa jicho la dunia nizidhihirishe; na hali njema ya roho iliyokandamizwa chini ya giza za tamaa za nafsi nionyeshe mfano wake; na nguvu za Mungu ambazo zikiingia ndani ya binadamu zinadhihirika kwa njia ya mwelekeo kwenye Mungu na dua nielezee kaifa yake kwa hali si kwa maneno tu; na zaidi ya hayo yote ni hii kuwa imani halisi katika Umoja wa Mungu inayong'aa isiyochanganyika na aina yoyote ya ushirikina, ambayo hivi sasa haipo, niupande mche wake wa kudumu ndani ya taifa. Haya yote hayatakuwa kwa nguvu yangu bali yatakuwa kwa nguvu ya yule Mungu ambaye ni Mungu wa mbingu na ardhi. Mimi naona kuwa Mungu upande mmoja akinilea kwa mkono wake na kunifunulia wahyi wake Ameujalia moyo wangu jazba hii kwamba niinuke ili kurekebisha hali za namna hii, na upande wa pili Ameandaa mioyo pia ambayo ipo tayari kuyakubali maneno yangu. Naona kuwa tangu Mungu Aliponituma duniani kwa amri yake, kuanzia wakati ule mapinduzi makubwa yanaendelea kutokea duniani. Wale watu waliokuwa wanaupenda uungu

wa Hadhrat Isa[as] huko Ulaya na Marekani, sasa watafiti wao wenyewe wanaendelea kujitenga na itikadi hii. Na taifa ambalo tangu mababu zao walipenda sana masanamu na miungu, wengi wao wamepata kuelewa kwamba sanamu si chochote, si lolote. Na ingawa watu hao bado hawana habari na mambo ya kiroho na wameshikamana na maneno machache kama mazoea tu, lakini hakuna shaka kuwa wameondolea mbali shingoni mwao kamba za maelfu ya mila za kipuuzi, bidaa na ushirikina, na wamesimama karibu na mwingilio wa imani juu ya Umoja wa Mungu. Natumai baada ya muda mfupi, fadhili ya Mungu ikiwasukuma kwa mkono wake maalum itawaingiza wengi wao katika nyumba ya amani ya Tauhid ya kweli na kamili ambayo pamoja nayo mtu hujaaliwa mapenzi kamili, hofu kamili na utambuzi kamili. Matumaini yangu haya siyo mawazo tu, bali nimepata bishara hii kutokana na wahyi mtakatifu wa Mungu. Hekima ya Mungu imefanya kazi hii nchini humu ili Ayaunganishe mataifa mbalimbali haraka sana kuwa taifa moja na Alete siku ya suluhu na amani. Kila mmoja anaipata harufu nzuri ya hewa hii kuwa mataifa haya yote mbalimbali siku moja yatakuwa taifa moja. Wakristo wanaeneza mawazo haya kuwa hivi karibuni dini ya dunia nzima itakuwa hii kwamba watu watamwamini Hadhrat Isa[as] kuwa Mungu. Na Mayahudi wanaoitwa Banii Israeli nao siku hizi wameingiwa na jazba mpya kuwa Masihi wao maalumu atakayewarithisha ardhi nzima atakuja katika siku hizi hizi. Kadhalika bishara za Islam pia zinazoahidi ujaji wa Masihi mmoja, muda wa ahadi yake pia unaishia kwenye karne ya kumi na nne ya Hijiria. Na Waislamu wa kawaida pia wanafikiri kuwa zama zipo karibu ambapo Uislamu

utaenea kote ardhini. Nimewasikia baadhi ya Mapanditi wa Sanatan Dharm kuwa zama za kudhihiri Autari mmoja (nabii wao) ni zama hizi hizi. Na wanasema kuwa huyu ndiye Autari wa mwisho ambaye kwa njia yake dini itaenea duniani kote. Na Waariya ingawa hawasemi kuna utabiri wowote, hata hivyo kutokana na athari ya upepo unaovuma, wao pia wanajibidiisha na kujaribu dini yao ienee Asia, Ulaya, Marekani, Japani na kadhalika. Na ajabu zaidi ni kwamba hata wafuasi wa dini ya Kibudha pia wameingiwa upya na jazba hiyo. Na jambo la kuchekesha ni kuwa hata matopasi wa nchi hii pia wanahangaika kuwa kwa njia yoyote wao wasalimike katika kunyanyaswa na kunyonywa na mataifa mengine, na kwa uchache waweze kupata nguvu ya kulinda dini yao. Ilmuradi, katika zama hizi umevuma upepo kwamba kila kundi linataka kwa jazba sana maendeleo ya taifa lake na ya dini yake, na wanataka hata alama ya mataifa mengine isibakie tena. Bali wao tu ndio wabaki. Na kama vile wakati wa dhoruba ya bahari mawimbi yanavyopigapiga moja juu ya jingine, ndivyo hivyo dini mbalimbali zinavyoshambuliana. Kwa vyovyote, kutokana na harakati hizi inahisiwa kuwa hizi ni zile zile zama ambamo Mwenyezi Mungu Amenuia kuyaunganisha makundi mbalimbali kuwa kaumu moja, na Akimaliza magomvi haya ya kidini awakusanye wote kwenye dini moja. Na kuhusu zama hizi ambazo ni zama za dhoruba ya mawimbi, Mwenyezi Mungu Amesema ndani ya Kurani Tukufu:

وَنُفِخَ فِي الصُّوْرِ فَجَمَعْنٰهُمْ جَمْعًا ۝ [33]

[33] Al-Kahaf: 100

Aya hii pamoja na aya za awali zinamaanisha kwamba zama ambamo dini zilizo duniani zitakuwa na vurugu nyingi, na kila dini itaishambulia dini nyingine kama vile wimbi linavyoangukia wimbi jingine na zitataka kuangamizana, hapo Mungu wa mbingu na ardhi katika zama zile za dhoruba Ataanzisha Jumuiya mpya kwa mikono yake bila kutumia njia za kidunia na Atawakusanya humo wote wawezao na wafaao, ndipo watatambua dini ni kitu gani, na watapuliziwa uhai na roho ya unyofu wa kweli na watanyweshwa kikombe cha utambuzi wa Mungu. Na ni lazima dunia isikome kuendelea mpaka bishara hii itimie iliyoelezwa na Kurani Tukufu miaka elfu moja mia tatu tangu leo. Na kuhusu zama hizi za mwisho ambamo mataifa yote yatakusanywa kwenye dini moja Mungu Hakueleza alama moja tu, bali katika Kurani Tukufu mmeandikwa pia alama nyingine kadha. Katika hizo mojawapo ni kwamba katika zama zile mifereji mingi itatoka kutoka katika mito; na nyingine tena ni hii kwamba migodi mingi iliyofichika, yaani madini, itachimbuliwa na elimu nyingi za kidunia zitadhihirika. Na nyingine ni kwamba njia zitapatikana zitakazofanya vitabu viongezeke (hii inaashiria kwenye mitambo ya uchapishaji). Alama nyingine ni kwamba itapatikana njia fulani ya usafiri itakayowafanya ngamia wasifae, na kwa sababu yake njia za kukutana zitakuwa rahisi; na mojawapo ni kwamba mawasiliano hapa duniani yatakuwa rahisi na wataweza kufikishana taarifa za habari kwa urahisi. Nyingine tena ni kwamba katika siku zile katika mwezi mmoja, jua na mwezi vitapatwa huko mbinguni; na nyingine ni kwamba baada ya hapo tauni kali sana itaenea ardhini hata kwamba hakuna mji wala kijiji kitakachosalia bila

kuingiliwa na tauni, na vifo vingi vitatokea duniani, na dunia itabaki tupu. Baadhi ya vijiji vitaangamia kabisa na hazitabaki alama zao, na baadhi ya vijiji baada ya kuadhibiwa kiasi fulani vitaokolewa. Siku zile zitakuwa siku za adhabu kali ya Mungu, kwa sababu watu hawatazikubali ishara za Mungu zidhihirikazo kwa Mjumbe wake wa zama zile, watamkataa Nabii wa Mungu ajaye kurekebisha watu na watamkadhibisha. Alama zote hizo zimetimia katika zama hizi. Kwa mwenye akili, njia iko safi na wazi kuwa Mungu Amenituma katika wakati ambapo alama zote zilizoandikwa na Kurani Tukufu zimedhihirika kwa ujaji wangu. Alama zote hizi zinazohusu zama za Masihi Aliyeahidiwa, ingawa zimo ndani ya Hadithi pia, lakini hapa nimetoa Kurani Tukufu tu. Kuna alama moja nyingine kuhusu zama za Masihi Aliyeahidiwa ambayo Kurani Tukufu imeeleza katika sehemu moja kuwa:

اِنَّ يَوْمًا عِنْدَ رَبِّكَ كَاَلْفِ سَنَةٍ مِّمَّا تَعُدُّوْنَ ○ [34]

Yaani kuna siku moja ya Mungu ambayo ni sawa na miaka yenu elfu moja. Kwa vile siku zenyewe ni saba, hivyo katika aya hii umri wa dunia umehesabiwa kuwa miaka elfu saba, lakini umri huo ni kutoka zama za Adam ambaye sisi ni uzao wake. Kutokana na Neno la Mungu inaonekana kuwa hapo kabla pia dunia ilikuwepo. Hatuwezi kusema kuwa watu wale walikuwa kina nani na walikuwa wa aina gani. Inaonekana awamu moja ya dunia huisha katika miaka elfu saba, ndiyo maana kwa sababu hiyo na kwa ajili ya kuliwekea alama jambo hili, siku saba zimewekwa duniani ili kila siku iashirie kwenye

[34] Al-Hajj:48

miaka elfu moja. Hatujui kuwa awamu ngapi za aina hiyo zimekwisha pita duniani na ma-Adam wangapi wamekwisha tokea katika zama zao. Kwa kuwa Mungu ni Mwumbaji tangu azali, hivyo tunakubali na tunaamini kwamba dunia yenyewe ni ya tangu kale, lakini siyo kwamba haina Mwumbaji. Ni masikitiko kwamba Wakristo wana itikadi kuwa miaka elfu sita tu imepita tangu Mungu Alipoiumba dunia na kutengeneza ardhi na mbingu; eti kabla ya hapo Mungu sikuzote Alikaa bure tu, hakufanya kazi, wala hakuwa na kazi tangu azali.

Hii ni itikadi ambayo mwenye akili yeyote hataikubali. Lakini itikadi yetu ambayo Kurani Tukufu imetufundisha ni kuwa Mungu ni Mwumbaji tangu azali; Akitaka Anaweza kuziangamiza ardhi na mbingu mara mamilioni kisha Azitengeneze kama zilivyo. Na imetuhabarisha kuwa yule Adam aliyekuja baada ya nyimati za awali alikuwa baba yetu sote. Tangu afike duniani kipindi hiki cha kibinadamu kikaanza, na muda kamili wa umri wa kipindi hiki ni mpaka miaka elfu saba. Miaka hii elfu saba kwa Mungu ni kama siku saba za wanadamu. Ikumbukwe kuwa kanuni ya Mungu imepanga kwamba kipindi kwa kila umati huwa cha miaka elfu saba. Kwa kuashiria kwenye kipindi hicho, siku saba zimepangwa kwa ajili ya wanadamu. Ilmuradi kipindi cha umri wa mwanadamu kimewekwa cha miaka elfu saba; na katika hiyo karibu miaka elfu tano ilikuwa imekwisha pita katika zama za ujaji wa Nabi wetu[saw], au tuseme kwa maneno mingine kwamba kutoka katika siku za Mungu, siku tano zilikwishapita tayari kama Alivyoashiria ndani ya Kurani Tukufu katika Sura 'Al-Asr', yaani katika herufi zake sawa na abjadi,

kwamba katika uhai wa Mtume[saw]. sura hii ilipoteremka, muda kiasi hiki ulikuwa umekwisha pita tangu zama za Adam ambao ni dhahiri katika thamani ya herufi za sura hiyo. Kwa hesabu hii, kutoka katika umri wa mwanadamu sasa miaka elfu sita imekwishapita na imebaki miaka elfu moja. Katika Kurani Tukufu bali hata katika vitabu vya zamani pia imeandikwa kuwa mjumbe wa mwisho atakayekuja katika sura ya Adam na ataitwa kwa jina la Masihi, ni lazima azaliwe mwishoni mwa miaka elfu sita kama vile Adam alivyozaliwa mwishoni mwa siku ya sita. Alama hizi zote zinatosha kwa mwenye kuzingatia. Na mgawanyiko wa miaka hii elfu saba kwa mujibu wa Kurani Tukufu na Vitabu vingine vya Mungu ni hivi kwamba elfu ya kwanza ni zama za kuenea wema na mwongozo, na elfu ya pili ni zama za utawala wa shetani; na elfu ya tatu ni ya kuenea wema na mwongozo, na elfu ya nne ni ya utawala wa shetani; na kisha elfu ya tano ni ya kuenea wema na mwongozo. (Hiyo ndiyo elfu ambamo Seyyidna wa Maulana, Mbora wa mitume, Hadhrat Muhammad[saw] alitumwa kuja kurekebisha ulimwengu na shetani akafungwa jela.) Na tena elfu ya sita ni zama za shetani kufunguliwa na kutawala, zinazoanzia baada ya karne tatu na kuishia mwanzoni mwa karne ya kumi na nne. Na kisha elfu ya saba ni ya Mungu na Masihi wake na ni zama za heri na baraka ya aina zote, imani na urekebisho, ucha-Mungu na Umoja wa Mungu, ibada ya Mungu na kila aina ya wema na mwongozo. Sasa tupo mwanzoni mwa elfu ya saba. Baada ya hapo hakuna tena nafasi kwa Masihi mwingine kuja, maana zama zenyewe ni saba tu zilizogawanywa katika wema na ubaya. Mgawanyo huu umeelezwa na manabii wote,

wengine wameeleza kwa muhtasari na wengine kwa kirefu. Na maelezo hayo yamo katika Kurani Tukufu ambayo kutokana na hayo inaonekana kwa uwazi sana kwamba bishara kuhusu Masihi Aliyeahidiwa imo katika Kurani Tukufu. Na ni jambo la ajabu kwamba manabii wote wanazungumzia katika vitabu vyao zama za Masihi kwa njia hii au ile na pia wanaelezea fitina za dajali. Na hakuna bishara yoyote duniani iliyotabiriwa kwa nguvu na kusimuliwa kwa njia nyingi tofauti kama walivyotabiri manabii wote kuhusu Masihi wa mwisho. Hata hivyo, wanapatikana pia watu katika zama hizi wanaoukataa usahihi wa bishara hii. Baadhi yao wanasema thibitishieni bishara hii kutoka ndani ya Kurani Tukufu. Lakini ni masikitiko kuwa kama wangefikiria vizuri Kurani Tukufu au kuizingatia, wangelazimika kukiri kuwa bishara hii imo ndani ya Kurani Tukufu kwa uwazi sana, na ni wazi kiasi hiki kwamba mtu mwenye busara hahitaji maelezo zaidi ya hayo. Imeashiriwa ndani ya sura 'At-Tahrim' kuwa baadhi ya watu katika umati huu wataitwa ibn Mariamu, kwani kwanza wamefananishwa na Mariamu kisha imeelezwa kwamba watapuliziwa roho kama Mariamu. Neno hili linaashiria kuwa kwanza wakiwa na umbo la Kimariamu (kiroho) watapata maendeleo, kisha watakuwa ibn Mariamu, kama Mwenyezi Mungu Alivyoniita kwanza Mariamu katika wahyi uliomo ndani ya *Barahine Ahmadiyya* na Akasema:

يَا مَرْيَمُ اسْكُنْ اَنْتَ وَ زَوْجُكَ الْجَنَّةَ

"Ewe Mariamu, wewe na rafiki zako ingieni peponi", kisha Akasema

يَا مَرْيَمُ نَفَخْتُ فِيْكَ مِنْ رُّوْحِ الصِّدْقِ

yaani, ewe Mariamu, Mimi nimekupulizia roho ya ukweli (kana kwamba kwa njia ya istiara Mariamu akapata himila ya "ukweli"), kisha akasema mwishoni:

يَا عِيسٰى اِنِّىْ مُتَوَفِّيْكَ وَ رَافِعُكَ اِلَيَّ

yaani, ewe Isa, Mimi nitakufisha na nitakuinua kwangu. Basi, hapa mimi nikihamishwa kutoka daraja la Kimariamu nikapewa jina la Isa, na kwa njia hii nikafanywa mwana wa Mariamu, ili itimie ile ahadi iliyoelezwa ndani ya sura 'At-Tahriim'. Kadhalika imeelezwa ndani ya sura 'An-Nuur' kuwa Makhalifa wote watatokea kutoka katika umati huu huu. Na inathibitika kutoka ndani ya Kurani Tukufu kuwa umati huu utafikiwa na zama mbili za kutisha; zama moja zilizowadia katika enzi ya Ukhalifa wa Abubakr[ra] baada ya kifo cha Mtume[saw], na zama za pili ni zama za fitina ya dajjal iliyokadiriwa kutokea katika zama za Masihi ambayo aya hii inaashiria kujikinga nayo.

غَيْرِ الْمَغْضُوْبِ عَلَيْهِمْ وَلَا الضَّآلِّيْنَ○ [35]

Na kuhusu zama hizo hizo, ndani ya sura 'An-Nuur' mna bishara hii:

وَلَيُبَدِّلَنَّهُمْ مِّنْ بَعْدِ خَوْفِهِمْ اَمْنًا [36]

Muradi wa aya pamoja na aya iliyopita ndio huu kwamba Mwenyezi Mungu Anasema kuwa katika zama za mwisho dini hii itapatwa na matetemeko, na

35 Al-Fatiha :7

36 An-Nuur:56

itahofiwa isije dini hii ikatoweka duniani kote, ndipo Mwenyezi Mungu Ataiimarisha dini hii juu ya uso wa ardhi mara ya pili, na Ataleta amani baada ya hofu, kama Anavyosema ndani ya aya nyingine kuwa:

هُوَ الَّذِيۡۤ اَرۡسَلَ رَسُوۡلَهٗ بِالۡهُدٰى وَ
دِيۡنِ الۡحَقِّ لِيُظۡهِرَهٗ عَلَى الدِّيۡنِ كُلِّهٖ [37]

Yaani, Mungu ndiye yule Mungu Aliyemtuma Mtume wake ili aishindishe dini ya Islam juu ya dini zote. Hii pia inaashiria kwenye zama za Masihi Aliyeahidiwa. Kisha kuna aya hii:

اِنَّا نَحۡنُ نَزَّلۡنَا الذِّكۡرَ وَ اِنَّا لَهٗ لَحٰفِظُوۡنَ ○ [38]

Hii pia inaashiria kwenye zama za Masihi Aliyeahidiwa. Na kwa mujibu wa Kurani Tukufu zama za Masihi Aliyeahidiwa zinafanana na zama za Hadhrat Abubakr[ra] Kwa wenye akili wanaotafakari uthibitisho huu wa Kurani Tukufu ni wenye kutuliza. Na kama hayo hayatoshi machoni mwa jahili yeyote, basi hapo yampasa akiri kwamba hakuna bishara yoyote katika Torati  kumhusu Hadhrat Isa[as] wala hamna utabiri wowote kumhusu Mtume wetu[saw], maana maneno yale pia yameelezwa kwa muhtasari. Na ndiyo sababu Mayahudi wakajikwaa na hawakumkubali. Kwa mfano, kama bishara kumhusu Mtume Mtukufu[saw] ingetolewa kwa maneno ya wazi wazi kabisa kuwa yeye atazaliwa mjini Makka na jina lake lenye baraka litakuwa Muhammad, na jina la baba yake litakuwa Abdullah na jina la babu yake litakuwa Abdul Muttalib, naye atatokana na ukoo wa

---

[37] As-Saf 10

[38] Al-Hijr:10

Bani Ismail, na atahamia Madina na atazaliwa miaka kadhaa baada ya nabii Musa[as], kwa alama hizo hakuna Myahudi ambaye angeweza kukataa. Na kuhusu bishara ya ujaji wa Yesu, Wayahudi walipatwa na matatizo mengi zaidi ambayo kwayo wanajifikiria wana udhuru kweli. Maana, bishara inayomhusu Hadhrat Masihi ndiyo kwamba Masihi huyo hatadhihiri mpaka Eliya arejee mara ya pili duniani; lakini Eliya hajafika mpaka sasa. Na ndani ya Kitabu cha Mungu ilikuwa sharti kuwa Masihi wa kweli atakayekuja kutoka kwa Mungu, hakuna budi kabla yake Eliya aje mara nyingine dunani. Jibu kutoka kwa Hadhrat Masihi lilikuwa kwamba muradi wa neno hili ni ujaji wa mfano wa Eliya na siye Eliya mwenyewe. Lakini Wayahudi wanasema kuwa huku ni kubadili maneno ya Mungu; sisi tulipewa habari ya kuja mara ya pili kwa Eliya mwenyewe. Hii inaonyesha kuwa bishara zinazowahusu manabii daima huwa nzito, ili kwayo tofauti ibainike kati ya mwenye bahati mbaya na mwenye bahati njema.

Aidha, ni dhahiri kuwa madai ya kweli hayana uthibitisho wa aina moja tu, bali kama almasi halisi ambayo katika jiha zake zote mnatoka mwanga, madai hayo nayo hung’aa kwa kila jiha. Basi nasema kwa nguvu kuwa madai yangu ya mimi kuwa Masihi Mau‘udi ndiyo yenye shani hii kwamba yanang’aa kwa kila jiha. Kwanza angalieni upande huu kuwa madai yangu ya mimi kutoka kwa Mungu na kupata heshima ya kuongea na Mungu ni ya tangu miaka karibu ishirini na saba, yaani muda mrefu sana hata kabla *Barahine Ahmadiyya* kilikuwa hakijaandikwa. Kisha wakati wa *Barahine Ahmadiyya* kutungwa, madai hayo yakiandikwa katika kitabu hicho

yakaenzwa, na tangu hapo karibu miaka ishrini na minne imekuwisha pita. Sasa mtu mwenye busara anaweza kufahamu kuwa uongu hauwezi kuendelea kwa muda mrefu kiasi hiki; na mtu hata kama ni mwongo mkubwa namna gani, hawezi kitabia kutenda uovu kama huo kwa muda mrefu abamo mtoto baada ya kuzaliwa anaweza kupata wazao. Aidha, hakuna mtu mwenye akili anayeweza kulikubali kuwa mtu mmoja kwa zaidi ya miaka ishirini na saba anaendelea kumzulia Mwenyezi Mungu uongo, kila asubuhi anazua ufunuo na anazibuni bishara na kuzinasibisha kwa Mwenyezi Mungu, na kila siku anadi kuwa Mwenyezi Mungu Amenifunulia ufunuo huu na haya ndiyo maneno ya Mwenyezi Mungu yaliyoniteremkia, ilhali Mungu Anajua kuwa yu mwongo katika jamabo hilo, hakufunuliwa kamwe wala Mungu hakuongea naye na Mungu anamchukulia kuwa mtu mlaaniwa lakini hata hivyo Anamsaidia na Jumuiya yake Anaipa maendeleo, na Anamnusurisha na njama zote na mabalaa yote wanayompangia wapinzani. Kisha kuna dalili moja nyingine inayoonesha ukweli wangu wazi wazi na kuja kwangu kutoka kwa Mungu kunathibitika. Nayo ndiyo hii kuwa katika zama zile ambapo kulikuwa hakuna mtu aliyenijua, yaani katika zama za *Barahine Ahmadiyya*, wakati nilipokuwa nakiandika kitabu hiki faraghani, na minghairi ya Mungu Aliye mjuzi wa mambo ya ghaibu hakuwa yeyote aliyejua hali yangu, katika zama hizo Mungu Akiongea nami Akatabiri matabiri kadha yaliyochapishwa ndani ya *Barahine Ahmadiyya* na kuenezwa katika hali ile ya upweke na umaskini nchini kote. Nayo ndiyo haya:

يَا اَحْمَدِیْ اَنْتَ مُرَادِیْ وَ مَعِیْ۔ سِرُّكَ سِرِّیْ۔ اَنْتَ مِنِّیْ بِمَنْزِلَةِ تَوْحِيْدِیْ وَ تَفْرِيْدِیْ۔ فَحَانَ اَنْ تُعَانَ وَ تُعْرَفَ بَيْنَ النَّاسِ۔ اَنْتَ مِنِّیْ بِمَنْزِلَةٍ لَّا يَعْلَمُهَا الْخَلْقُ۔ يَنْصُرُكَ اللّٰهُ فِیْ مَوَاطِنَ۔ اَنْتَ وَجِيْهٌ فِیْ حَضْرَتِیْ اِخْتَرْتُكَ لِنَفْسِیْ۔ وَ اِنِّیْ جَاعِلُكَ لِلنَّاسِ اِمَامًا۔ يَنْصُرُكَ رِجَالٌ نُّوْحِیْ اِلَيْهِمْ مِّنَ السَّمَآءِ۔ يَاْتِيْكَ مِنْ كُلِّ فَجٍّ عَمِيْقٍ۔ يَاْتُوْنَ مِنْ كُلِّ فَجٍّ عَمِيْقٍ۔ وَ لَا تُصَعِّرْ لِخَلْقِ اللّٰهِ وَلَا تَسْئَمْ مِّنَ النَّاسِ۔ وَ قُلْ رَّبِّ لَا تَذَرْنِیْ فَرْدًا وَّ اَنْتَ خَيْرُ الْوَارِثِيْنَ۔ اَصْحَابُ الصُّفَّةِ وَ مَا اَدْرَاكَ مَا اَصْحَابُ الصُّفَّةِ۔ تَرٰی اَعْيُنَهُمْ تَفِيْضُ مِنَ الدَّمْعِ رَبَّنَآ اِنَّنَا سَمِعْنَا مُنَادِياً يُّنَادِیْ لِلْاِيْمَانِ۔ اِنِّیْ جَاعِلُكَ فِی الْاَرْضِ خَلِيْفَةً۔ يَقُوْلُوْنَ اَنّٰی لَكَ هٰذَا۔ قُلِ اللّٰهُ عَجِيْبٌ۔ لَا يُسْئَلُ عَمَّا يَفْعَلُ وَ هُمْ يُسْئَلُوْنَ۔ وَ يَقُوْلُوْنَ اِنْ هٰذَآ اِلَّا اخْتِلَاقٌ۔ قُلِ اللّٰهُ ثُمَّ ذَرْهُمْ فِیْ خَوْضِهِمْ يَلْعَبُوْنَ۔ هُوَ الَّذِیْ اَرْسَلَ رَسُوْلَهٗ بِالْهُدٰی وَدِيْنِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهٗ عَلَی الدِّيْنِ كُلِّهٖ۔ يُرِيْدُوْنَ اَنْ يُّطْفِئُوْا نُوْرَ اللّٰهِ وَ اللّٰهُ مُتِمُّ نُوْرِهٖ وَلَوْ كَرِهَ الْكَافِرُوْنَ۔ يَعْصِمُكَ اللّٰهُ وَ لَوْ لَمْ يَعْصِمْكَ النَّاسُ۔ اِنَّكَ بِاَعْيُنِنَا سَمَّيْتُكَ الْمُتَوَكِّلَ۔ وَ مَا كَانَ اللّٰهُ لِيَتْرُكَكَ حَتّٰی يَمِيْزَ الْخَبِيْثَ مِنَ الطَّيِّبِ۔ شَاْتَانِ تُذْبَحَانِ وَ كُلُّ مَنْ عَلَيْهَا فَانٍ۔ وَ عَسٰی اَنْ تَكْرَهُوْا شَيْئًا وَّ هُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ وَ عَسٰی اَنْ تُحِبُّوْا شَيْئًا وَّ هُوَ شَرٌّ لَّكُمْ وَ اللّٰهُ يَعْلَمُ وَ اَنْتُمْ لاَ تَعْلَمُوْنَ۔

Tafsiri: Mungu akiongea nami Anasema: Ewe Ahmad wangu, u kusudio langu, na u pamoja nami. Siri yako ni siri yangu. U kwangu kama Umoja wangu na kuwa kwangu wa pekee. Basi wakati upo karibu watakapotayarishwa watu wa kukusaidia, na utafanywa ujulikane baina ya watu. Una cheo na daraja kwangu ambayo dunia haiijui. Mungu

Atakusaidia katika kila medani. Wewe una heshima kwangu, Mimi nimekuchagua kwa ajili yangu, Nitawafanya watu wengi kuwa watiifu na wafuasi wako, nawe utafanywa imamu wao. Mimi Nitawafunulia mioyoni mwa watu ili wakusaidie kwa mali zao. Kutoka njia za mbali na zitakazokuwa na mashimo-mashimo kwa sabau ya kukanyagwa sana misaada ya kifedha itakufikia. Kutoka njia za mbali watu watakujia. Hivyo unalazimika usiwatendee vibaya wala usichoke kwa wingi wao na kuja kwa makundi kwa makundi. Na uwe unaomba dua hii kuwa: Ewe Mungu wangu, Usiniache peke yangu na hakuna mrithi bora kuliko Wewe. Mungu Ataandaa kwa ajili yako watu wa Suffa. Na je, unajua watu wa Suffa ni kina nani? Utawaona machozi yakiwadondoka nao watasema: Ee Mungu wetu, sisi tumesikia sauti ya mwitaji anayewaita watu kwenye imani. Mimi nitakufanya wewe Khalifa ardhini. Watu wanasema kwa dharau kuwa unawezaje kukipata cheo hiki? Waambie kuwa Mungu yule ni Mungu mwenye kudra za ajabu. Kazi Anayofanya Yeye, hakuna awezaye kuhoji kwa nini Umefanya hivyo. Naye Atamshika kila mmoja kwa kauli yake kuwa kwa nini umesema hivi. Na wanasema kuwa huu ni uzushi tu. Wajibu kuwa Mungu ndiye Mwanzilishi wa kazi hii; kisha uwaache katika michezo yao. Mungu ndiye yule Mungu Aliyemtuma Mjumbe wake kwa mwongozo na dini ya haki ili aishindishe dini hii juu ya dini zote. Watu hao watanuia kuizima nuru ambayo Mungu Anataka kuieneza duniani, lakini Mungu Ataikamilisha nuru hii, yaani Ataifikisha kwenye mioyo yenye bidii, ijapokuwa makafiri wakirihike. Mungu Atakulinda na shari yao, ingawa watu wasiweze kulinda. U mbele ya macho yangu.

Nimekupa jina 'Mutawakil' (mwenye kumtegemea Mungu), na Mungu si mwenye kukuacha mpaka Aonyeshe tofauti baina ya safi na mchafu. Mbuzi wawaili watachinjwa, na yeyote aliyopo ardhini mwishoni atakufa tu. Huenda mchukie kitu nacho ni heri kwenu; na huenda mkipende kitu nacho ni shari kwenu. Na Mwenyezi Mungu Anajua kitu gani kinawafaeni nanyi hamjui.

Sasa ieleweke kuwa ndani ya funuo hizi zimeelezwa bishara nne kubwa sana. (1) Moja ndiyo hii kuwa wakati nilipokuwa peke yangu wala hakuna yeyote aliyekuwa pamoja nami, katika zama hizo ambapo miaka karibu ishirini na mitatu imekwisha pita sasa, Mwenyezi Mungu Alinipa habari njema kwamba wewe hutabakia peke yako, na wakati waja, bali u karibu, ambapo watu makundi kwa makundi watakuwa pamoja nawe; nao watakujia kutoka njia za mbali, na watakuja kwa wingi kiasi hiki hata kwamba huenda ukachoka nao, au kuwatendea vibaya; lakini usifanye hivyo. (2) Bishara ya pili ni hii kuwa utapatikana msaada mkubwa wa mali kutoka kwa watu hao. Watu wengi ni mashahidi wa bishara hizo kuwa zilipoandikwa hizo ndani ya *Barahine Ahmadiyya*, mimi nilikuwa peke yangu katika Qadian, kijiji kisichokuwa na watu wengi, katika hali ya kutojulikana, lakini baada ya hapo hata miaka kumi ilikuwa haijapita, watu wakawa wanaeleka kwangu kwa mujibu wa ufunuo wa Mwenyezi Mungu, na pia kwa mali zao watu wakaanza kutoa misaada, hata kwamba hivi sasa watu zaidi ya laki mbili wameishafanya baiati kwangu. Na bishara ya tatu iliyomo ndani ya funuo hizo ni kuwa watu watajaribu kuifutilia mbali Jumuiya hii na kuizima

nuru hii, lakini watashindwa katika juhudi hii. Sasa, kama mtu ang'ang'anie kukataa, nani anayeweza kumzuia? Waila bishara hizo tatu zinang'aa mithili ya jua. Ni dhahiri kuwa katika zama ambapo mtu awe anaishi bila kujulikana, yu peke yake bila msaidizi yeyote, na hakuna alama yoyote ya yeye kufanywa kiongozi wa malaki ya watu, na wala hakuna dalili yoyote kuwa watu watamletea maelfu ya rupia, hapo katika hali kama hiyo ikiwa inawezekana kutabiri kumhusu mtu huyo kupata ufanisi na msaada wa Mungu hivyo kwa kutumia akili tu na kubahatisha, basi mkana anapaswa alete mfano wake kwa kutaja jina, hususan bishara hizo mbili zinapounganishwa na bishara hiyo ya tatu inayomaanisha kuwa watu watajaribu sana ili bishara hizi zisitimie, lakini Mungu Atazitimiza. Basi kwa kuziangalia bishara hizo tatu kwa pamoja itakuwa hakuna budi kukubali kuwa hii siyo kazi ya mwanadamu. Mwanadamu hawezi hata kudai kuwa ataweza kuishi mpaka muda fulani. Kisha bishara ya nne katika funuo hizo ni hii kuwa katika muda huu wafuasi wawili wa Jumuiya hii watauawa katika njia ya Mungu. Basi Sheikh Abdur Rahman kwa amri ya Amir Abdur Rahman mtawala wa Kabul, na Maulawii Sahibzada Abdul Latif Khan kwa idhini ya Amir Habibullah, waliuawa katika njia ya Mungu.

Mbali na hizo, kuna mamia ya bishara zilizotimia katika nyakati zake. Safari moja Maulawii Hakim Nuruddin alipashwa habari kabla ya wakati kuwa atajaaliwa mwana ambaye mwilini mwake vitakuwa vipele kadhaa. Ndivyo ilivyotokea. Mtoto yule wa kiume akazaliwa na mwilini mwake kulikuwa na vipele. Bwana Maulawii yupo katika mkutano huu,

mtu yeyote anaweza kumwuliza aeleze kwa kula kiapo kuwa je, jambo hili ni kweli au hapana. Tena, mwanaye Sardar Muhammad Ali Khan, Mkuu wa Malir Kotla, jina lake Abdur Rahim, aliugua, alama za kukata tamaa zikadhihirika, na Mungu kwa ufunuo akanipasha habari kuwa mtoto huyu anaweza kupona kwa maombezi yako. Basi, mimi nikiwa mwongozi mwenye huruma nikamwombea sana dua, na mtoto huyo akapona, kana kwamba mfu akafufuka. Kisha vivyo hivyo mwanaye wa pili Abdullah Khan naye akaugua, yeye pia akaugua maradhi hatari ya kutisha na akakurubia kufa. Nikaambiwa kuhusu kupona kwake pia, naye akapona kwa maombi yangu.

Kadhalika zipo ishara nyingine nyingi; kama zote ziandikwe haiyumkiniki madhumuni haya yaweze kumalizika hata katika siku kumi. Mashahidi wa ishara hizo si mmoja au wawili, bali malaki ya watu ni mashahidi. Miongoni mwa ishara hizo, ishara mia moja na hamsini nimeziandika ndani ya kitabu changu kiitwacho '*Nuzuulul – Masihi*' ambacho kitatoka hivi karibuni. Ishara zile zote ni za aina nyingi. Baadhi yake zilidhihiri mbinguni na baadhi yake ardhini, baadhi yake kuhusu marafiki na baadhi yake kuhusu maadui, zilizokwisha timia; baadhi yake zinanihusu mimi na baadhi yake zinawahusu wazao wangu. Na zipo baadhi ya ishara ambazo zimedhihirika kwa sababu ya adui fulani bila mimi kuingilia kati, kama Sheikh Ghulam Dastagir wa Kasur aliyefanya mwenyewe mubahala nami katika kitabu chake '*Fat-he Rahman*' na akaomba kuwa yeyote miongoni mwetu wawili aliye mwongo, Mungu Amhilikishe. Basi siku chache tu zilipita baada ya dua hii, Sheikh huyo mwenyewe akafa, na

kwa kifo chake akatoa ushahidi juu ya ukweli wangu. Na kuna maelfu ya watu ambao kwa njia ya ndoto pekee, Mwenyezi Mungu Aliwadhihirishia ukweli wangu. Ilimuradi, ishara hizo ziko wazi sana hata kwamba kama zikiangaliwa kwa ujumla, mtu anakuwa hana budi kukubali. Baadhi ya wapinzani wa zama hizi wanasema pia kuwa ikithibitika kutoka ndani ya Kurani Tukufu sisi tutakubali. Mimi ninawajibu kwa kusema kuwa ndani ya Kurani Tukufu mna uthibitisho wa kutosha juu ya mimi kuwa Masihi, kama nilivyokwisha andika pia kiasi fulani.

Isitoshe, kuleta tu sharti hii ni kutumia tu nguvu na kupiga ubwana. Kumkubali mtu yeyote kuwa mkweli siyo lazima habari zake zipatikane wazi wazi ndani ya kitabu fulani kilichofunuliwa. Kama sharti hili ni la lazima, basi unabii wa nabii yeyote hautathibitika. Ukweli wenyewe ni huu kuwa mtu akidai kuwa nabii, kwanza kabisa inaangaliwa kwamba je, zama zinahitaji nabii? Kisha inaangaliwa pia kuwa je, huyo amefika katika wakati uliotabiriwa na manabii au la. Kisha inatazamiwa pia kwamba Mungu Amemsaidia au la. Kisha hii pia inaangaliwa kuwa je, shutuma walizoleta maadui zimejibiwa vilivyo au hapana. Mambo hayo yote yanapotimia, itakubaliwa kwamba mtu huyo ni mkweli waila hapana. Sasa, ni dhahiri kabisa kuwa zama zinatoa vilio kwa hali yake kwamba, kwa kuondoa mafarakano ya Waislamu, na kuinusuru Islam katika mashambulizi ya kutoka nje, na kuimarisha tena wema uliopotea, bila shaka kunahitajika mrekebishaji aje kutoka mbinguni ambaye kwa kuleta yakini tena aimwagilie maji mizizi ya imani, na kwa njia hii akiachisha maovu na dhambi awarejeshe watu kwenye ukweli. Basi, kuja

kwangu katika wakati hasa wa haja ni dhahiri hata kwamba siwezi kufikiri kuwa yeyote anaweza kukataa isipokuwa mwenye chuki sana. Na sharti la pili, yaani kuangalia kwamba je amekuja katika wakati uliotabiriwa na manabii au hapana, sharti hilo nalo limetimia kwa ujaji wangu. Maana, manabii walitabiri kwamba elfu ya sita itakapokaribia kwisha ndipo yule Masihi Aliyeahidiwa atadhihiri. Na elfu ya sita sawa na kalenda ya kimwezi kutokea Nabii Adam imekwisha malizika tangu zamani; na kwa mujibu wa kalenda ya kijua, elfu ya sita i karibu kumalizika. Zaidi ya hayo, Mtume wetu[saw] alisema kuwa mwanzoni mwa kila karne atatokea mujaddidi atakayejadidisha dini. Na sasa katika karne hii ya kumi na nne miaka ishirini na mmoja tayari imekwisha pita, na sasa mwaka wa ishirini na mbili ndio unaoendelea kupita. Sasa, je, hii siyo alama ya jambo hili kuwa mujaddidi yule ameisha fika? Na Sharti la tatu lilikuwa kuwa je, Mungu Amemsaidia pia au hapana. Sharti hili pia ni dhahiri limetimia kwangu. Kwani baadhi ya maadui wa kila kaumu ya nchi hii walidhamiria kuniangamiza na wakatumia nguvu yao yote na wakafanya bidii sana, lakini wakashindwa katika juhudi zao zote. Hakuna kaumu yoyote iliyojaaliwa fahari ya kuweza kusema kuwa miongoni mwetu kuna mtu yeyote ambaye hakufanya juhudi za aina yoyote ya kumwangamiza mtu huyu. Na kinyume cha juhudi zao, Mungu Akanipatia heshima na Akawafanya maelfu ya watu wanitii. Sasa, kama huu haukuwa msaada wa Mungu, ulikuwa ni nini basi? Nani hajui kuwa mataifa yote, kwa njia yao, walifanya mikakati ili waniangamize, lakini mimi sikuweza kuangamia kwa juhudi zao, bali nikazidi kupata maendeleo siku hadi siku, mpaka

Jumuiya yangu imefikia watu zaidi ya laki mbili. Basi, kama mkono uliofichikana wa Mungu usingekuwa nami, na kama shughuli zangu hizi zingekuwa ni mpango wa kibinadamu tu, bila shaka lazima katika mishale hiyo mshale mmojawapo ungelinipata na ningelikwisha angamia zamani sana, na leo isingekuwa hata alama ya kaburi langu. Kwani yule anayemtungia Mungu uongo, kumwangamiza yeye, njia nyingi hupatikana, kwani Mungu Mwenyewe Anakuwa adui yake. Lakini Mungu Akanikinga na njama zao zote kama Alivyonifahamisha miaka ishirini na minne hapo kabla. Zaidi ya hayo, huu ni msaada dhahiri namna gani kuwa katika zama za upweke wangu na kutojulikana kwangu, Mungu Akanipasha habari katika *Barahine Ahmadiyya* kwa maneno yaliyo wazi kuwa Mimi Nitakusaida na Nitakupa Jumuiya kubwa na Nitawafanya wapinzani washindwe kupata shabaha yao. Basi, fikirini kwa moyo safi kuwa msaada huu ni dhahiri namna gani na ni alama iliyo wazi namna gani!! Je, chini ya mbingu kuna mtu au shetani mwenye uwezo huu kwamba katika wakati wa kutojulikana atoe habari ya aina hii na itimie; na maelfu ya maadui wajitokeze lakini yeyote asiweze kuzuia kutimia habari hiyo. Kisha sharti la nne lilikuwa hili kuwa upinzani walioleta wapinzani, je upinzni huo wote umejibiwa kikamilifu au hapana. Sharti hili pia limetimia kwa uwazi sana, maana, upinzani mmoja mkubwa wa wapinzani ulikuwa kwamba Masihi Aliyeahidiwa ndiye Hadhrat Isa[as], yeye mwenyewe atakuja duniani mara ya pili. Basi, wakajibiwa ya kuwa inathibitika kutoka katika Kurani Tukufu kuwa Hadhrat Isa[as] ameishafariki na kamwe

hatarudi mara ya pili hapa duniani, kama Mungu Anavyosema Akitaja maneno yake (Nabii Isa[as]):

فَلَمَّا تَوَفَّيْتَنِيْ كُنْتَ اَنْتَ الرَّقِيْبَ عَلَيْهِمْ [39]

Kwa kuiunganisha na aya za awali tafsiri inakuwa hivi kuwa siku ya kiama Mwenyezi Mungu Atamwuliza nabii Isa[as] kuwa je, wewe ndiye uliyefundisha kuwa mimi na mama yangu tuaminini kuwa miungu wawaili na tuabuduni sisi. Yeye atasema kuwa Ee Mungu wangu! kama mimi nimesema hivyo, Wewe Unajua, kwani Wewe ni mjuzi wa mambo ya ghaibu; mimi niliwaambia yale tu Uliyoniambia, yaani aminini kuwa Mungu ni Mmoja, Hana mshirika, na mimi ni Mtume wake. Mimi nilikuwa najua hali zao nilipokuwa ndani yao, lakini Uliponifisha, Wewe Ukawa shahidi juu yao, mimi sijui kuwa baada yangu walifanya nini! Sasa, kutokana na aya hizi, ni dhahiri kuwa nabii Isa[as] atajibu kuwa mimi nilipokuwa hai Wakristo hawakuharibika; na nilipokufa, sijui hali yao ilikuwaje. Basi, kama ikubaliwe kuwa Hadhrat Isa[as] mpaka sasa yu hai, itabidi papo hapo tuamini kuwa mpaka sasa Wakristo nao hawajaharibika na wako imara juu ya dini ya kweli. Zaidi ya hayo, katika aya hii Hadhrat Isa[as] anaeleza hana habari ya baada ya kifo chake na anasema kuwa: Ee Mungu wangu, Uliponifisha, tanagu wakati huo sijui hali ya wafuasi wangu. Hivyo basi, kama habari hii ikubaliwe kuwa ni sahihi kuwa kabla ya kiama yeye atakuja duniani, na akiungana na Mahdi atapigana na makafiri, hapo aya hii ya Kurani Tukufu itabatilika, Mungu Atupishe

[39] Al-Maida : 118

mbali, au inabidi kukubali kuwa Hadhrat Isa[as] siku ya kiama atasema uongo mbele ya Mungu, na ataficha habari hii kuwa yeye alirudi mara ya pili duniani, na akaishi miaka arobaini na akiungana na Mahdi akapigana na Wakristo. Hivyo, kama kuna mwenye kuiamini Kurani Tukufu, basi ajue kwamba kutokana na aya hii moja tu mpango wote unathibitika kuwa batili ya kwamba Mahdi mwuaji atazaliwa na Masihi atakuja kumsaidia kutoka mbinguni. Mtu mwenye itikadi hii bila shaka anaiacha Kurani Tukufu. Kisha wapinzani wetu wanaposhindwa katika kila jambo, mwishoni husema kuwa baadhi ya bishara zangu hazijatimia, kama vile bishara kumhusu Atham. Mimi nasema kuwa Atham yuko wapi sasa? Kiini cha bishara hii kilikuwa kwamba mtu aliye mwongo atakufa katika uhai wa mkweli; basi Atham amekufa, na mimi mpaka sasa niko hai. Bishara hiyo ilikuwa na masharti, yaani muda wake wa kutimia uliambatana na sharti. Basi, kwa kuwa Atham akiisha sikia bishara alidumu kutishika, akatimiza sharti hilo, ndiyo maana akaongezewa muda wa miezi michache. Ni sikitiko kuwa waletao upenzani huu hawazingatii kwamba bishara ya Nabii Yunus[as] aliyotoa haikuwa na sharti lolote kama ilivyoandikwa ndani ya kitabu cha Yona, hata hivyo bishara hiyo haikutimia. Ukweli wenyewe ni kwamba bishara za onyo, yaani bishara zenye ahadi ya kumwadhibu mtu huwa siku zote na masharti ya kufanya toba au kutoa sadaka au inaambatana na kuogopa, na zinaweza kuahirishwa au kuondolewa kabisa kwa kufanya toba, kuomba ghofira, kutoa sadaka na kumwogopa Mwenyezi Mungu. La sivyo, nabii Yunus hawezi kuthibitika kuwa nabii; maana bishara yake isiyokuwa na sharti haikutimia. Nia za adhabu ya Mungu zinazomhusu

mkosefu zinaweza kutanguka kwa kutoa sadaka pia na kufanya maombi pia; na hata kwa kuogopa pekee pia zaweza kutanguka. Hivyo basi, bishara inayohusikana na adhabu, maana yake ni hii tu kuwa Mwenyezi Mungu Amefunga nia ya kumuadhibu mtu fulani, na nia hiyo Amemdhihirishia pia nabii fulani. Basi, kwa nini nia hiyo yaweza kutanguka kwa kutoa sadaka na kuomba ambapo nabii fulani hakupashwa habari yake, lakini akiisha pashwa habari, hapo isiweze kutanguka? Wazo hili ni ujinga mtupu, na ni kuwapinga manabii wote. Zaidi ya hayo, baadhi za bishara zaelezwa kwa ufupi na nyingine zinakuwa na maana zaidi ya moja ambazo uhakika wake hujulikana baadaye. Na hii pia ni kweli kuwa pengine katika kuieleza bishara fulani nabii anaweza kukosea, na hiyo haidhuru, maana, nabii pia ni binadamu. Hadhrat Isa[as] alisema kuwa wafuasi wangu kumi na wawili watakaa peponi katika viti kumi na viwili vya enzi, lakini hiyo haikuthibitika kuwa sahihi, kwani mfuasi mmoja aliritadi, akastahili kwenda motoni. Na alisema kuwa watu wa zama hizi watakuwa wangali hai nitakaporudi mara ya pili. Habari hii pia haikutokea kuwa sahihi. Na kuna matabiri mengine ya Hadhrat Isa[as] ambayo hayakuweza kutimia kutokana na ukosefu wa kuyaelewa. Ilmuradi, haya yalikuwa ni makosa ya kuelewa muradi wake. Na hali ya bishara zangu ni hii kuwa kama kuna msikilizaji asikilizaye kwa subira na kutaka ukweli, basi zipo bishara na ishara zaidi ya laki moja zilizodhihirika kunisaidia. Basi, ni ufidhuli wa hali ya juu kutonufaika kabisa na maelfu ya bishara zilizokwisha timia, na kama mojawapo haikuweza kueleweka, hiyo ifanywe kitovu cha ubishi, na yapigwe makelele, na shauri zima liamuliwe kwa hiyo pekee. Mimi

natumaini na ninasema kwa yakini kamili kuwa kama mtu akae nami hata kwa siku arobaini, lazima atashuhudia ishara. Sasa namaliza na nina yakini kuwa haya yanatosha kwa ajili ya mtafuta haki.

وَ السَّلَامُ عَلٰى مَنِ اتَّبَعَ الْهُدٰى [40]

Mwandishi;

**Mirza Ghulam Ahmad**

**wa Qadian**.

[40] Na amani iwe kwa yule anayefuata mwongozo.

# NYONGEZA

Bwana mmoja, Hakim Mirza Mahmud Mwirani, ameuliza leo Septemba 2, 1902, katika barua yake kuwa aya hii ina maana gani:

وَجَدَهَا تَغۡرُبُ فِيۡ عَيۡنٍ حَمِئَةٍ [41]

Basi ibainike kuwa aya ya Kurani ina siri nyingi sana ndani yake, nayo haiwezi kueleweka kikamilifu ambapo chini ya maana yake ya dhahiri kuna maana ya ndani pia. Lakini muradi wake alionidhihirishia Mungu ni huu kwamba aya hii pamoja na za kabla yake na za baada yake ni bishara kumhusu Masihi Aliyeahidiwa, na inaainisha wakati wa kudhihiri kwake. Na maelezo yake ni kwamba Masihi Aliyeahidiwa pia ni Dhulkarnain. Kwani *'karn'* katika lugha ya Kiarabu ni 'karne' na aya ya Kurani inaashiria kwamba Masihi wa ahadi atakayedhihiri wakati fulani, kuzaliwa kwake na kudhihiri kwake kuwa Masihi itakuwa katika karne mbili, na hivi ndivyo nilivyo mimi. Kuwepo kwangu kumetokea namna ambavyo nimepata karne mbili maarufu za kalenda zote, iwe ya Hijriya au ya Kikristo au ya Kibikarmajiti (ya Kibaniani). Kuzaliwa kwangu na kudhihiri kwangu hakukuishia karne moja tu sawa na kalenda yoyote. Ilmuradi, nijuavyo mimi, kuzaliwa kwangu na kudhihiri kwangu hakuishii karne moja tu sawa na kalenda ya dini yoyote, bali huingia katika karne mbili. Basi kwa maana hii mimi ni Dhulkarnain. Hata ndani ya baadhi ya Hadithi pia Masihi Aliyeahidiwa ameitwa Dhulkarnain. Katika

[41] Al-Kahf : 87

Hadithi hizo pia maana ya Dhulkarnain ni ile ile niliyoielezea. Sasa tafsiri ya aya iliyobaki kwa mujibu wa bishara ni hii kuwa duniani kuna mataifa mawili makubwa yaliyopewa habari njema ya Masihi Aliyeahidiwa na hayo ndiyo yamepewa haki ya kwanza kuitwa na Masihi. Basi hapa Mwenyezi Mungu Anasema kwa njia ya istiara kuwa Masihi Mau‘di ambaye ndiye Dhulkarnain, atakuta katika safari yake mataifa mawili. Ataliona taifa moja limekaa katika giza kwenye chemchem inayonuka ambayo maji yake hayafai kunywewa, ndani yake mna matope yanukayo sana na ni kiasi cha kuyafanya yasiitwe sasa maji. Hili ni taifa la Kikristo ambalo liko gizani ambalo kwa makosa yake limechanganya chemchem ya Masihi katika matope yanukayo.

Katika safari ya pili, Masihi Mau‘di ambaye ni Dhulkarnain akawaona watu waliokaa katika jua kali, hakuna kinga baina yao na jua. Wao hawakupata mwanga wowote wa jua bali wamepata sehemu hii tu kwamba inaungua miili yao hata ngozi ya juu imekuwa nyeusi. Watu hao ndio Waislamu ambao wako mbele ya jua, lakini hawakufaidika kitu ila kuungua tu. Yaani wao walijaaliwa jua la Tauhidi, lakini hawakujipatia nuru ya kweli ya jua hata kidogo, isipokuwa wakapata kuungua tu. Yaani, wao wamepoteza uzuri wa kweli wa kidini na hulka njema, nao wakawa na chuki, inda, ukali na mwendo wa kinyama. Kwa kifupi ni kwamba kwa njia hii Mwenyezi Mungu Anasema kwamba Masihi Aliyeahidiwa ambaye ni Dhulkarnain atakuja wakati ambapo Wakristo watakuwa gizani, wao watapata matope yanayonuka yanayoitwa kwa lugha ya Kiarabu *Hama’*, (matope meusi); na Waislamu

watakuwa na Tauhid kavu tu mkononi, na watakuwa wameungua kwa jua la chuki na unyama, na hali yao ya kiroho haitakuwa safi. Kisha Masihi ambaye ndiye Dhulkarnain atalikuta taifa lingine la tatu litakalokuwa limesumbuliwa sana na Yajuja na Majuja, na watu hao watakuwa wenye kushika sana dini, na tabia zao zitakuwa nzuri, na hao wataomba msaada kutoka kwa Dhulkarnain ambaye ndiye Masihi Aliyeahidiwa ili waepukane na mashambulio ya Yajuja na Majuja, na atawatengenezea kinga iliyo wazi, yaani atawafundisha hoja madhubuti za kuisaidia Islam na atakomesha kabisa mashambulizi ya Yajuja na Majuja. Na atapangusa machozi yao na atawasaidia kwa kila njia, na atakuwa pamoja nao. Hii inaashiria kwa wale wanaonikubali mimi. Hii ndiyo bishara yenye shani kubwa, na humu habari imetolewa kinagaubaga juu ya kudhihiri kwangu, wakati wa ujaji wangu na kuhusu Jumuiya yangu. Basi, amebarikiwa yule anayesoma bishara hizo kwa makini. Kawaida ya Kurani Tukufu ni kuwa inatoa bishara za namna hii pia ya kwamba anayezungumzwa ni mtu fulani lakini shabaha inakuwa kutoa bishara kwa siku zijazo. Kama vile katika sura Yusuf pia kuna bishara ya namna hiyo, yaani, kidhahiri kisa kimoja kimeelezwa, lakini kuna bishara iliyofichika ndani yake kuwa kama vile nduguze Yusufu kwanza walivyomwangalia yeye kwa jicho la dharau, lakini mwishowe Yusufu huyo huyo akawa kiongozi wao, ndivyo hivyo itakavyokuwa kwa Makuraishi. Na kweli watu hao walimkataa Mtume[saw] na kumfukuza katika Makka, lakini yule yule aliyekataliwa akafanywa kiongozi na mkuu wao.

Ni mahali pa kustaajabia kuwa mara nyingi sana ndani ya Kurani Tukufu bishara zimeelezwa kumhusu Masihi Aliyeahidiwa yaani mimi, hata hivyo baadhi ya watu ambao hawana busara wanasema kwamba katika Kurani Tukufu hakuna habari yoyote kumhusu Masihi Aliyeahidiwa. Hao watu ni kama Wakristo amabo mpaka sasa wanasema kwamba katika Biblia hakuna bishara yoyote kumhusu Mtume wa Mungu[saw]

(Tafsiri ya beti za Kiajemi)

*Macho yapo wazi, na masikio pia ya wazi,*
*Na fahamu nayo ipo; nashangaa Mungu*
*Alivyoyafanya macho yasione.*
*Ewe uliyetayarisha upinde na mishale,*
*Windo li karibu, ukaitupa mbali.*

Mwandishi,

**Mirza Ghulam Ahmad**

**wa Qadian**.